# Hisabati

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Tatu



Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Hisabati

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Tatu

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1220

Jina la Chapisho: Hisabati Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-996-2

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 1 Novemba 2023 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Tatu katika Ngazi ya Elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2023.

**Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa**
Kamishna wa Elimu

FOR ONLINE USE ONLY

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2018
Chapa ya Pili 2021
Toleo la Pili 2023

ISBN: 978-9987-09-996-2

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 35094
14112 Dar es Saalam

Simu: +255735041170/+255735041168
Barua pepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

Shukurani ..... iv

Utangulizi ..... vi

**Sura ya Kwanza**
Namba nzima ..... 1

**Sura ya Pili**
Kujumlisha na kutoa namba nzima ..... 48

**Sura ya Tatu**
Vipimo vya urefu, uzani na ujazo ..... 77

**Sura ya Nne**
Maumbo ..... 93

**Sura ya Tano**
Sehemu ..... 110

**Sura ya Sita**
Vipimo vya muda ..... 131

**Sura ya Saba**
Fedha ya Tanzania ..... 153

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

*Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki kutoka taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali zilizoshiriki kufanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi. Kipekee, TET inatoa shukurani kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Chuo Kikuu cha Ardhi, Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, vyuo vya ualimu na shule za msingi. Pia, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:*

**Waandishi:** Dkt. Kenneth R. Nzowa, Bi. Ivy P. Bimbiga, Bw. Anthony K. Tresphory, Dkt. Angela R. Katabaro na Bi. Skolastika A. Kulanga

**Wahariri:** Dkt. Michael H. Mkwizu, Dkt. Augustino I. Msigwa, Dkt. Ahmada O. Ali, Bw. Luwilo D. Sanga, Bw. Elikana E. Manyilizu na Dkt. Zubeda S. Mussa

**Msanifu:** Bi. Eva G. Kwai

**Wachoraji:** Bw. Fikiri A. Msimbe, Bi. Victoria R. Mwinyi, Bw. Godwin J. Chipenya na Bw. Gwakisa U. Mwandoloma

**Mratibu:** Dkt. Kenneth R. Nzowa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vilevile, TET inatoa shukurani kwa walimu wote wa shule za msingi na wanafunzi walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Mwisho, TET inaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha zilizofanikisha kazi ya uandishi na uchapishaji wa kitabu hiki.



Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki cha Hisabati kimetayarishwa mahususi kwa ajili ya mwanafunzi wa Darasa la Tatu, Tanzania Bara. Kitabu hiki kimeandaliwa kwa kulingana na Muhtasari wa somo la Hisabati Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mwaka 2023. Aidha, kitabu hiki ni Toleo la Pili lililoboreshwa kutoka kitabu cha Hisabati Darasa la Tatu kilichochapishwa mwaka 2018 kwa kuzingatia muhtasari wa mwaka 2016.

Kitabu hiki kina sura saba ambazo ni namba nzima, kujumlisha na kutoa namba nzima, vipimo vya urefu, uzani na ujazo, maumbo, sehemu, vipimo vya muda na fedha ya Tanzania. Kwa kujifunza maudhui ya kitabu hiki, utakuza umahiri wa kumudu misingi ya awali ya kihisabati na kutumia stadi za kihisabati katika kufikiri kimantiki, kutafsiri na kutatua matatizo ya maisha ya kila siku.

Maudhui ya sura hizi yamewasilishwa njia ya matini, michoro, picha pamoja na kazi za vitendo. Unashauriwa kufanya kazi zote na mazoezi yote yaliyomo katika kitabu hiki, pamoja na kazi nyingine utakazopewa na mwalimu. Hii itakuwezesha kukuza maarifa na stadi zinazokusudiwa kwa mwanafunzi.

Jifunze zaidi kupitia maktaba mtandao

https://ol.tie.go.tz au ol.tie.go.tz

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sura ya Kwanza

# Namba nzima

**Utangulizi**

*Katika sura hii, utajifunza namba nzima zenye tarakimu zaidi ya moja. Utabaini thamani ya nafasi ya tarakimu na thamani ya tarakimu katika namba nzima, utajifunza kusoma na kuandika namba nzima. Vilevile, utalinganisha namba nzima na kubainisha mfuatano katika namba nzima. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia namba nzima katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na maisha ya kila siku kama vile vipimo, fedha na biashara.*

## Thamani ya nafasi ya tarakimu katika namba nzima

Kila nafasi ya tarakimu katika namba nzima ina thamani yake. Thamani ya nafasi ya tarakimu katika namba nzima huongezeka kutoka kulia kuelekea kushoto. Thamani ya nafasi ya tarakimu katika namba nzima huwakilishwa kama ifuatavyo:

(a) Nafasi ya kwanza kutoka kulia huwakilisha **mamoja**.

(b) Nafasi ya pili kutoka kulia huwakilisha **makumi**.

(c) Nafasi ya tatu kutoka kulia huwakilisha **mamia**.

(d) Nafasi ya nne kutoka kulia huwakilisha **maelfu**.

(e) Nafasi ya tano kutoka kulia huwakilisha **makumi elfu**.

(f) Nafasi ya sita kutoka kulia huwakilisha **mamia elfu**.

(g) Nafasi ya saba kutoka kulia huwakilisha **mamilioni**.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Mfano wa 1

Andika thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba 1364.

**Jibu**

4 ni mamoja
6 ni makumi
3 ni mamia
1 ni maelfu

### Mfano wa 2

Andika thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba 6948.

**Jibu**

8 ni mamoja
4 ni makumi
9 ni mamia
6 ni maelfu

### Mfano wa 3

Ikiwa tarakimu katika maelfu ni 7, katika mamia ni 3, katika makumi ni 0 na katika mamoja ni 4, je, hii ni namba gani?

**Jibu**

7304

### Mfano wa 4

Jaza nafasi zilizoachwa wazi:

5463 ina maelfu___, mamia___, makumi___ na mamoja___.

**Jibu**

5463 = maelfu 5, mamia 4, makumi 6 na mamoja 3.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Mfano wa 5

Onesha thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba nzima zifuatazo:


(a) 4628 (b) 3456 (c) 7304 (d) 9000

**Njia**


(a) 4628





(b) 3456




(b) 7304




(c) 9000




## Zoezi la 1

1. Andika tarakimu ya kila thamani ya nafasi katika namba 9825 katika nafasi zilizo wazi.
   (a) _____ ipo thamani ya nafasi ya makumi.
   (b) _____ ipo thamani ya nafasi ya mamoja.
   (c) _____ ipo thamani ya nafasi ya maelfu.
   (d) _____ ipo thamani ya nafasi ya mamia.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Andika namba nzima ambayo ina thamani ya nafasi ya tarakimu zifuatazo:
   (a) 2 iwe mamia, 9 mamoja, 3 maelfu na 8 makumi.
   (b) 0 iwe mamoja, 2 mamia, 6 makumi na 5 maelfu.
   (c) 6 iwe makumi, 6 maelfu, 8 mamia na 2 mamoja.
   (d) 3 iwe maelfu, 4 makumi, 8 mamia na 7 mamoja.

3. Jaza jedwali lifuatalo kuonesha thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba nzima.

| **Namba** | **Thamani ya nafasi ya tarakimu** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Maelfu** | **Mamia** | **Makumi** | **Mamoja** |
| 1001 | | | | |
| 6666 | | | | |
| 4000 | | | | |
| 3339 | | | | |

4. (a) Katika 7029, ni tarakimu ipi ipo katika thamani ya nafasi ya mamia?
   (b) Katika 8173, ni tarakimu ipi ipo katika thamani ya nafasi ya maelfu?
   (c) Taja tarakimu inayochukua thamani ya nafasi ya makumi katika 3487.
   (d) Ikiwa tarakimu katika makumi ni 6 na tarakimu katika mamia ni 7, je, hii ni namba gani?

5. (a) Kuna mamia mangapi katika namba 3287?
   (b) Katika kikapu kuna tufaa 9674. Je, katika kikapu hicho kuna maelfu mangapi ya tufaa?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Bainisha thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba zifuatazo:

(a) 6247 (b) ९९९९ (c) 7001

(d) 4444 (e) 3239 (f) 2776

(g) 1111 (h) 8107 (i) ९००९

(j) 5108

7. Andika thamani ya nafasi ya tarakimu yenye kivuli katika namba zifuatazo:

(a) 10**2**0 (b) **2**010 (c) 168**7**

(d) 7**९**22 (e) 888**8** (f) 1**6**९2

(g) **5**401 (h) ९1**1**1 (i) 3**3**33

(j) 20**0**0

8. Jaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kuandika thamani ya nafasi ya tarakimu katika namba zifuatazo:

(a) २९६८

2 ipo katika thamani ya nafasi ya _____,

९ ipo katika thamani ya nafasi ya _____,

6 ipo katika thamani ya nafasi ya _____,

8 ipo katika thamani ya nafasi ya _____.

(b) ९८०1

९ ipo katika thamani ya nafasi ya _____,

8 ipo katika thamani ya nafasi ya _____,

0 ipo katika thamani ya nafasi ya _____,

1 ipo katika thamani ya nafasi ya _____.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) 7236

7 ipo katika thamani ya nafasi ya _____,
2 ipo katika thamani ya nafasi ya _____,
3 ipo katika thamani ya nafasi ya _____,
6 ipo katika thamani ya nafasi ya _____.

(d) 5649

5 ipo katika thamani ya nafasi ya _____,
6 ipo katika thamani ya nafasi ya _____,
4 ipo katika thamani ya nafasi ya _____,
9 ipo katika thamani ya nafasi ya _____.

9. Andika namba nzima inayowakilishwa na thamani ya nafasi ya tarakimu katika jedwali lifuatalo:

| Maelfu | Mamia | Makumi | Mamoja | Namba |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 0 | 2 | 0 | |
| 1 | 1 | 2 | 0 | |
| 2 | 4 | 4 | 0 | |
| 3 | 3 | 0 | 1 | |
| 6 | 8 | 9 | 9 | |
| 9 | 2 | 7 | 4 | |
| 2 | 9 | 7 | 3 | |
| 8 | 1 | 2 | 2 | |
| 7 | 1 | 7 | 3 | |
| 1 | 2 | 7 | 7 | |
| 7 | 2 | 9 | 1 | |
| 1 | 0 | 0 | 0 | |
| 2 | 3 | 1 | 1 | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

10. Jaza tarakimu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

(a) 1872 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(b) 2663 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(c) 4793 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(d) 5187 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(e) 4002 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(f) 1562 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(g) 7371 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(h) 4572 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(i) 3421 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(j) 2012 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(k) 6682 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(l) 5583 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(m) 5234 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(n) 2709 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(o) 5235 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(p) 9123 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

(q) 3410 ina maelfu _____, mamia _____, makumi _____ na mamoja _____.

11. Andika tarakimu ambayo ina thamani ya nafasi ya maelfu katika namba zifuatazo:

(a) 7682 (b) 9501

(c) 8306 (d) 6412

12. Andika thamani ya nafasi ya tarakimu 3 katika namba zifuatazo:

(a) 436 (b) 3900

(c) 2843 (d) 2301

13. Pigia mstari kwenye tarakimu yenye thamani ya nafasi ya mamia katika namba zifuatazo:

(a) 269 (b) 7901

(c) 3749 (d) 9568

14. (a) Mimi ni namba nzima yenye tarakimu mbili. Nina tarakimu 3 katika mamoja na tarakimu katika makumi inazidi mamoja kwa 4. Je, mimi ni namba gani?


(b) Mimi ni namba nzima yenye tarakimu mbili. Nina tarakimu 9 katika makumi, na tarakimu katika mamoja ni pungufu kwa 3 katika makumi. Mimi ni namba gani?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuandika thamani ya nafasi ya tarakimu katika namba nzima kwa kutumia abakasi

Thamani ya nafasi ya tarakimu katika namba nzima inaweza kubainishwa kwa kutumia abakasi. Picha ifuatayo inaonesha wanafunzi wakiweka vihesabio katika abakasi ili kuunda namba nzima.




Baada ya kuunda namba nzima, wanaweza kubaini thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba nzima.

### Mfano wa 1

Andika thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika abakasi ifuatayo:

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE





**Jibu**

*Abakasi inawakilisha 4263.*

*Kuna maelfu 4, mamia 2, makumi, 6 na mamoja 3.*

## Mfano wa 2

*Andika thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika abakasi ifuatayo:*




**Jibu**

*Abakasi inawakilisha 5080.*


*Kuna maelfu 5, mamia 0, makumi 8 na mamoja 0.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 3

Andika thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika abakasi ifuatayo:




**Jibu**


Abakasi inawakilisha 6004.

Kuna maelfu 6, mamia 0, makumi 0 na mamoja 4.


## Zoezi la 2

Chunguza abakasi 1-6 kisha andika namba nzima zilizowakilishwa na abakasi hizo.

1.





2.





FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


3.





4.




5.




6.




7. *Tumia michoro ya abakasi kuwakilisha namba zifuatazo:*

(a) 4279 (b) 5802

(c) 6247 (d) 5108

## Thamani ya tarakimu katika namba nzima


*Thamani ya tarakimu katika namba nzima huongezeka kutoka kulia kuelekea kushoto. Hii ni thamani inayotafutwa kwa kuzingatia nafasi ya tarakimu husika katika namba nzima.*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 1

Andika thamani ya kila tarakimu katika namba ٩٦٧٢.

**Jibu**




## Mfano wa 2

Andika thamani ya tarakimu zilizopigiwa mstari katika namba ٨٧٩٤.

**Jibu**

Thamani ya 8 ni 8000 na thamani ya ٩ ni ٩٠.

## Mfano wa 3

Tumia namba٧٩٨٥ kuandika:

(a) thamani ya nafasi ya kila tarakimu.

(b) thamani ya kila tarakimu.

**Jibu**

| Namba | Tarakimu | Thamani ya nafasi ya tarakimu | Thamani ya tarakimu |
|---|---|---|---|
| ٧٩٨٥ | ٧ | Maelfu | ٧٠٠٠ |
| | ٩ | Mamia | ٩٠٠ |
| | 8 | Makumi | 80 |
| | 5 | Mamoja | 5 |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mfano wa 4**

Andika thamani ya nafasi ya tarakimu 6 na thamani ya tarakimu 4 katika 4612.

**Jibu**

Thamani ya nafasi ya tarakimu 6 katika 4612 ni mamia.
Thamani ya tarakimu 4 katika 4612 ni 4000.

## Zoezi la 3

1. Andika thamani ya tarakimu iliyopigiwa mstari katika namba nzima zifuatazo:
   (a) 4765 (b) 3926 (c) 1867
   (d) 4519

2. Andika thamani ya kila tarakimu katika namba nzima zifuatazo:
   (a) 2345 (b) 1246 (c) 8769
   (d) 9876

3. Andika thamani ya tarakimu 5 katika namba nzima zifuatazo:
   (a) 5672 (b) 3564 (c) 9851
   (d) 1695

4. Tumia namba 9864 kuandika:
   (a) thamani ya nafasi ya kila tarakimu.
   (b) thamani ya kila tarakimu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kufafanua namba nzima

Kufafanua namba nzima ni kuandika namba nzima katika thamani za tarakimu na kuzijumlisha. Utaratibu huu huonesha thamani ya kila tarakimu katika namba nzima. Namba nzima inapoandikwa kwa kifupi, thamani ya kila tarakimu katika namba hiyo inaweza kuandikwa kwa kufafanua namba hiyo.

### Mfano wa 1

Andika namba zifuatazo kwa kufafanua:

(a) 9732 (b) 5080 (c) 4000 (d) 3334

**Jibu**

(a) 9732 = 9000 + 700 + 30 + 2.

(b) 5080 = 5000 + 0 + 80 + 0.

(c) 4000 = 4000 + 0 + 0 + 0.

(d) 3334 = 3000 + 300 + 30 + 4.

### Mfano wa 2

Andika namba zifuatazo kwa kifupi:

(a) 4000 + 500 + 30 + 1 = (b) 4000 + 800 + 40 + 2 =

(c) 9000 + 700 + 0 + 2 = (d) 5000 + 0 + 0 + 1 =

**Jibu**

(a) 4000 + 500 + 30 + 1 = 4531.

(b) 4000 + 800 + 40 + 2 = 4842.

(c) 9000 + 700 + 0 + 2 = 9702.

(d) 5000 + 0 + 0 + 1 = 5001.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4


1. Andika namba nzima zifuatazo kwa kifupi:
   (a) 9000 + 800 + 70 + 2 =
   (b) 8000 + 800 + 80 + 0 =
   (c) 1000 + 0 + 0 + 6 =
   (d) 5000 + 600 + 50 + 8 =
   (e) 9000 + 700 + 0 + 2 =

2. Kamilisha jedwali lifuatalo. Mstari wa kwanza ni mfano.


| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8543 | = | 8000 | + | 500 | + | 40 | + | 3 |
| 3891 | = | | + | | + | | + | |
| 1654 | = | | + | | + | | + | |
| 4200 | = | | + | | + | | + | |
| 2901 | = | | + | | + | | + | |

3. Katika michoro (a) hadi (f), duara moja lina matawi manne yenye duara. Jumla ya thamani ya tarakimu zilizopo kwenye matawi ni sawa na namba nzima kwa kifupi. Jaza namba nzima zinazokosekana katika michoro hiyo. Swali la 3(a) ni mfano.

(a)





(b)





FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


(c)





(d)




(e)




(f)




4. Fafanua namba zifuatazo:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) | 7889 | (b) | 2043 | (c) | 8075 |
| (d) | 9690 | (e) | 3245 | (f) | 9770 |
| (g) | 3891 | (h) | 1654 | | |

## Kusoma na kuandika namba nzima

*Kusoma na kuandika namba nzima ni msingi wa kujifunza hisabati. Uandishi huo unahusisha kuandika namba kwa numerali ili kuwakilisha idadi ya vitu. Hapa utajifunza kusoma na kuandika namba nzima.*

### Kusoma namba nzima

*Kusoma namba nzima hutegemea wingi wa tarakimu hizo katika namba inayohusika. Anza kwa kubainisha mamoja, makumi, mamia, maelfu na kuendelea. Kisha soma kwa kuanzia*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kushoto kwenda kulia kwa kuzingatia thamani ya tarakimu iliyo kubwa. Kwa maana nyingine, anza na tarakimu iliyopo kwenye thamani ya nafasi kubwa kuliko zote.

### Mfano wa 1

Soma namba zifuatazo:

(a) 1001 (b) 1086 (c) 1100

**Jibu**

(a) 1001 husomwa elfu moja na moja.

(b) 1086 husomwa elfu moja na themanini na sita.

(c) 1100 husomwa elfu moja na mia moja.

### Zoezi la 5

Soma namba zifuatazo:

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1001 | 1002 | 1003 | 1004 | 1005 | 1006 | 1007 | 1008 | 1009 | 1010 |
| 1011 | 1012 | 1013 | 1014 | 1015 | 1016 | 1017 | 1018 | 1019 | 1020 |
| 1021 | 1022 | 1023 | 1024 | 1025 | 1026 | 1027 | 1028 | 1029 | 1030 |
| 1031 | 1032 | 1033 | 1034 | 1035 | 1036 | 1037 | 1038 | 1039 | 1040 |
| 1041 | 1042 | 1043 | 1044 | 1045 | 1046 | 1047 | 1048 | 1049 | 1050 |
| 1051 | 1052 | 1053 | 1054 | 1055 | 1056 | 1057 | 1058 | 1059 | 1060 |
| 1061 | 1062 | 1063 | 1064 | 1065 | 1066 | 1067 | 1068 | 1069 | 1070 |
| 1071 | 1072 | 1073 | 1074 | 1075 | 1076 | 1077 | 1078 | 1079 | 1080 |
| 1081 | 1082 | 1083 | 1084 | 1085 | 1086 | 1087 | 1088 | 1089 | 1090 |
| 1091 | 1092 | 1093 | 1094 | 1095 | 1096 | 1097 | 1098 | 1099 | 1100 |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 2

Soma namba zifuatazo:

(a) 1350 (b) 1572 (c) 9700

(d) 9540 (e) 9998

**Jibu**

(a) 1350 husomwa elfu moja mia tatu hamsini.

(b) 1572 husomwa elfu moja mia tano sabini na mbili.

(c) 9700 husomwa elfu tisa mia saba.

(d) 9540 husomwa elfu tisa mia tano arobaini.

(e) 9998 husomwa elfu tisa mia tisa tisini na nane.

## Zoezi la 6

Soma namba zilizomo katika jedwali lifuatalo:

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1100 | 1200 | 1300 | 1400 | 1500 | 1600 | 1700 | 1800 | 1900 | 2000 |
| 2100 | 2200 | 2300 | 2400 | 2500 | 2600 | 2700 | 2800 | 2900 | 3000 |
| 3100 | 3200 | 3300 | 3400 | 3500 | 3600 | 3700 | 3800 | 3900 | 4000 |
| 4100 | 4200 | 4300 | 4400 | 4500 | 4600 | 4700 | 4800 | 4900 | 5000 |
| 5100 | 5200 | 5300 | 5400 | 5500 | 5600 | 5700 | 5800 | 5900 | 6000 |
| 6100 | 6200 | 6300 | 6400 | 6500 | 6600 | 6700 | 6800 | 6900 | 7000 |
| 7100 | 7200 | 7300 | 7400 | 7500 | 7600 | 7700 | 7800 | 7900 | 8000 |
| 8100 | 8200 | 8300 | 8400 | 8500 | 8600 | 8700 | 8800 | 8900 | 9000 |
| 9100 | 9200 | 9300 | 9400 | 9500 | 9600 | 9700 | 9800 | 9900 | 10000 |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 7

1. Soma namba zifuatazo kwa ulalo na kwa wima:

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1110 | 1120 | 1130 | 1140 | 1150 | 1160 | 1170 | 1180 | 1190 | 1200 |
| 1210 | 1220 | 1230 | 1240 | 1250 | 1260 | 1270 | 1280 | 1290 | 1300 |
| 1310 | 1320 | 1330 | 1340 | 1350 | 1360 | 1370 | 1380 | 1390 | 1400 |
| 1410 | 1420 | 1430 | 1440 | 1450 | 1460 | 1470 | 1480 | 1490 | 1500 |
| 1510 | 1520 | 1530 | 1540 | 1550 | 1560 | 1570 | 1580 | 1590 | 1600 |
| 1610 | 1620 | 1630 | 1640 | 1650 | 1660 | 1670 | 1680 | 1690 | 1700 |
| 1710 | 1720 | 1730 | 1740 | 1750 | 1760 | 1770 | 1780 | 1790 | 1800 |
| 1810 | 1820 | 1830 | 1840 | 1850 | 1860 | 1870 | 1880 | 1890 | 1900 |
| 1910 | 1920 | 1930 | 1940 | 1950 | 1960 | 1970 | 1980 | 1990 | 2000 |

2. Soma namba zote zilizopo kwenye jedwali lifuatalo:

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1111 | 1112 | 1113 | 1114 | 1115 | 1116 | 1117 | 1118 | 1119 | 1120 |
| 1121 | 1122 | 1123 | 1124 | 1125 | 1126 | 1127 | 1128 | 1129 | 1130 |
| 1131 | 1132 | 1133 | 1134 | 1135 | 1136 | 1137 | 1138 | 1139 | 1140 |
| 1141 | 1142 | 1143 | 1144 | 1145 | 1146 | 1147 | 1148 | 1149 | 1150 |
| 1151 | 1152 | 1153 | 1154 | 1155 | 1156 | 1157 | 1158 | 1159 | 1160 |
| 1161 | 1162 | 1163 | 1164 | 1165 | 1166 | 1167 | 1168 | 1169 | 1170 |
| 1171 | 1172 | 1173 | 1174 | 1175 | 1176 | 1177 | 1178 | 1179 | 1180 |
| 1181 | 1182 | 1183 | 1184 | 1185 | 1186 | 1187 | 1188 | 1189 | 1190 |
| 1191 | 1192 | 1193 | 1194 | 1195 | 1196 | 1197 | 1198 | 1199 | 1200 |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Soma namba zifuatazo:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) | 6546 | (b) | 7865 | (c) | 2755 |
| (d) | 9118 | (e) | 4006 | (f) | 8009 |
| (g) | 7016 | (h) | 9468 | | |

## Kuandika namba nzima

Namba nzima huandikwa kuanzia kushoto kwenda kulia kwa kuzingatia thamani ya nafasi ya tarakimu. Namba nzima huandikwa kwa numerali au kwa maneno. Namba kwa numerali huonesha tarakimu zote na thamani ya nafasi ya kila tarakimu kwenye namba nzima husika.

### Mfano wa 1

Andika namba zifuatazo kwa maneno:

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | 1000 | (b) | 1001 | (c) | 1002 | (d) | 1003 |
| (e) | 1004 | (f) | 1005 | (g) | 1006 | (h) | 1007 |
| (i) | 1008 | (j) | 1009 | (k) | 1010 | | |

**Jibu**

| | Namba kwa numerali | Namba kwa maneno |
|---|---|---|
| (a) | 1000 | Elfu moja |
| (b) | 1001 | Elfu moja na moja |
| (c) | 1002 | Elfu moja na mbili |
| (d) | 1003 | Elfu moja na tatu |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | | |
|---|---|---|
| (e) | 1004 | Elfu moja na nne |
| (f) | 1005 | Elfu moja na tano |
| (g) | 1006 | Elfu moja na sita |
| (h) | 1007 | Elfu moja na saba |
| (i) | 1008 | Elfu moja na nane |
| (j) | 1009 | Elfu moja na tisa |
| (k) | 1010 | Elfu moja na kumi |

## Mfano wa 2

Andika namba zifuatazo kwa maneno:

(a) 1018 (b) 4216 (c) 5691

**Jibu**

(a) Elfu moja na kumi na nane

(b) Elfu nne mia mbili kumi na sita

(c) Elfu tano mia sita tisini na moja

## Mfano wa 3

Andika namba zifuatazo kwa numerali:

(a) Elfu tatu mia moja hamsini na tano

(b) Elfu tatu mia sita na nane

(c) Elfu tisa mia nne kumi na mbili

**Jibu**

(a) 3155 (b) 3608 (c) 9412

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8

1. Chunguza jedwali lifuatalo kisha jaza nafasi zilizowazi. Mstari wa kwanza wa ulalo ni mfano.

| Maelfu | Mamia | Makumi | Mamoja | Namba kwa numerali | Namba kwa maneno |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 0 | 0 | 1 | 1001 | Elfu moja na moja |
| | | | | 1019 | |
| | | | | 7070 | |
| | | | | | Elfu moja mia tatu hamsini |
| | | | | 1572 | |
| | | | | 9540 | |
| 9 | 9 | 9 | 8 | | |
| | | | | 1086 | |
| 1 | 1 | 0 | 0 | | |
| | | | | 5102 | Elfu tano mia moja na mbili |

2. Andika namba zifuatazo kwa maneno:

(a) 1250 (b) 1393 (c) 7288
(d) 3425 (e) 4537 (f) 7998
(g) 9663 (h) 8888 (i) 9999
(j) 6660 (k) 3618 (l) 2222
(m) 9768 (n) 7808 (o) 3030

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Andika namba zifuatazo kwa numerali:

| | | |
|---|---|---|
| (a) | Elfu moja na kumi | |
| (b) | Elfu mbili mia moja sitini | |
| (c) | Elfu tatu mia sita kumi na nane | |
| (d) | Elfu nne mia saba sitini na tatu | |
| (e) | Elfu tano mia sita themanini na tatu | |
| (f) | Elfu saba | |
| (g) | Elfu tisa mia mbili thelathini na tano | |
| (h) | Elfu sita mia moja ishirini na mbili | |
| (i) | Elfu tisa mia tisa sabini na tatu | |
| (j) | Elfu nane | |
| (k) | Elfu nane mia nane tisini na mbili | |
| (l) | Elfu tatu mia tano themanini na saba | |

4. Jaza nafasi zilizoachwa wazi katika jedwali lifuatalo:

| **Namba kwa numerali** | **Namba kwa maneno** |
|---|---|
| | Elfu moja na hamsini na mbili |
| 1201 | |
| | Elfu mbili |
| 3000 | |
| | Elfu nne mia tatu |
| 4506 | |
| | Elfu tano mia tano hamsini |
| 6000 | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| | Elfu sita mia sita |
| 7001 | |
| | Elfu nane na themanini |
| 9010 | |
| | Elfu tisa mia saba |

5. (a) Weka alama ya vema (✓) iwapo ni sahihi au weka alama ya mkasi (✗) iwapo sio sahihi katika jedwali lifuatalo. Mstari wa kwanza wa ulalo ni mfano.

| Namba kwa numerali | Namba kwa maneno | Alama |
|---|---|---|
| 6000 | Elfu sita | ✓ |
| 3618 | Elfu tatu mia sita kumi na nane | |
| 7288 | Elfu saba mia nane ishirini na nane | |
| 3435 | Elfu tatu mia nne hamsini na tatu | |
| 5633 | Elfu tano mia sita thelathini na tatu | |
| 9009 | Mia tisa na elfu tisa | |
| 6660 | Elfu sita sitini na mia sita | |
| 2086 | Elfu 2 na themanini na sita | |
| 3239 | Elfu tatu ishirini na tatu na tisa | |
| 2776 | Elfu mbili mia saba sabini na sita | |
| 7304 | Elfu saba na nne | |

(b) Andika kwa usahihi namba ulizoweka alama (✗) katika swali la 5(a).

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. *Chunguza kielelezo namba 1 na 2, soma maelezo yake, kisha jibu maswali yanayofuata.*



**Kielelezo namba 1:** *Jengo la Ngome Kongwe lililopo Zanzibar lilijengwa mwaka elfu moja mia sita tisini na tisa*



**Kielelezo namba 2:** *Mlima Kilimanjaro una urefu wa meta elfu tano mia nane tisini na tano*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

(a) Andika kwa numerali namba ulizosoma.

(b) Andika thamani ya nafasi ya kila tarakimu ya namba ulizosoma.

## Kusoma na kuandika namba nzima zinazozidi 10000

Idadi ya vitu inayozidi 10000 inaweza kuhesabiwa kwa urahisi kwa kutumia mafungu. Vilevile, ili kusoma na kuandika namba nzima zinazozidi elfu kumi kwa urahisi anza kubaini thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba nzima husika.

### Mfano wa 1

Andika thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba 61270, kisha andika namba hiyo kwa maneno.

**Jibu**

0 ipo thamani ya nafasi ya mamoja,

7 ipo thamani ya nafasi ya makumi,

2 ipo thamani ya nafasi ya mamia,

1 ipo thamani ya nafasi ya maelfu,

6 ipo thamani ya nafasi ya makumi elfu.

Kwa hiyo, namba 61270 inaandikwa sitini na moja elfu mia mbili sabini.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Mfano wa 2

Andika namba 876543 kwa thamani ya nafasi ya kila tarakimu, kisha andika namba hiyo kwa maneno.

**Jibu**

3 ipo thamani ya nafasi ya mamoja,

4 ipo thamani ya nafasi ya makumi,

5 ipo thamani ya nafasi ya mamia,

6 ipo thamani ya nafasi ya maelfu,

7 ipo thamani ya nafasi ya makumi elfu,

8 ipo thamani ya nafasi ya mamia elfu.

Kwa hiyo, namba 876543 inaandikwa mia nane sabini na sita elfu mia tano arobaini na tatu.

### Mfano wa 3

Andika thamani ya nafasi ya tarakimu katika namba 9261514 kisha andika kwa maneno.

**Jibu**

4 ipo thamani ya nafasi ya mamoja,

1 ipo thamani ya nafasi ya makumi,

5 ipo thamani ya nafasi ya mamia,

1 ipo thamani ya nafasi ya maelfu,

6 ipo thamani ya nafasi ya makumi elfu,

2 ipo thamani ya nafasi ya mamia elfu,

9 ipo thamani ya nafasi ya mamilioni.

Kwa hiyo, namba 9261514 inasomwa milioni tisa mia mbili sitini na moja elfu mia tano kumi na nne.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 4

Andika namba zifuatazo kwa kirefu:

(a) 24765 (b) 273453 (c) 2261514

**Jibu**

(a) 24765 = 20000 + 4000 + 700 + 60 + 5.

(b) 273453 = 200000 + 70000 + 3000 + 400 + 50 + 3.

(c) 2261514 = 2000000 + 200000 + 60000 + 1000 + 500 + 10 + 4.

## Mfano wa 5

Andika namba zifuatazo kwa numerali:

(a) Kumi na tatu elfu mia moja hamsini na tano

(b) Milioni moja mia tisa themanini elfu mia tatu tisini na tano

**Jibu**

(a) 13155 (b) 1980395

## Mfano wa 6

Andika namba 9876543 kwa kutumia thamani ya kila tarakimu

**Njia**

| Namba nzima | Tarakimu | Thamani ya tarakimu |
|---|---|---|
| 9876543 | 9 | 9000000 |
| | 8 | 800000 |
| | 7 | 70000 |
| | 6 | 6000 |
| | 5 | 500 |
| | 4 | 40 |
| | 3 | 3 |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 9


1. Andika namba zifuatazo kwa maneno:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) | 28749 | (b) | 38951 | (c) | 76187 |
| (d) | 97000 | (e) | 311008 | (f) | 7896246 |
| (g) | 89365 | (h) | 50050 | (i) | 821834 |
| (j) | 31425 | (k) | 200512 | (l) | 3437000 |

2. Andika namba zifuatazo kwa numerali:
   (a) Thelathini na tano elfu mia sita kumi na moja
   (b) Elfu sabini
   (c) Tisini elfu mia tisa na nane
   (d) Themanini elfu mia mbili na saba
   (e) Mia moja ishirini na saba elfu mia tisa
   (f) Mia nane elfu na nane
   (g) Milioni nane mia saba tisini elfu mia saba sabini na tisa
   (h) Milioni moja na mia tatu arobaini
   (i) Milioni tano mia tisa tisini na tisa elfu mia nne hamsini na sita


3. Tumia michoro ya abakasi ifuatayo kuandika namba zinazowakilishwa na michoro hiyo:

   (a)



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b)




4. Andika thamani ya nafasi ya 6 katika namba zifuatazo:
   (a) 645218 (b) 446128 (c) 21610
   (d) 699222 (e) 364974 (f) 239364

5. Andika thamani ya tarakimu iliyopigiwa mstari katika namba zifuatazo:
   (a) 49002 (b) 6249356 (c) 541341
   (d) 4755964 (e) 7215549 (f) 36314

6. Fafanua namba zifuatazo:
   (a) 79684 (b) 645218 (c) 8321483

7. Andika namba zifuatazo kwa kifupi:
   (a) 60000 + 5000 + 400 + 30 + 2
   (b) 800000 + 70000 + 6000 + 0 + 20 + 9
   (c) 7000000 + 600000 + 40000 + 5000 + 400 + 30 + 7

8. Andika thamani ya nafasi ya tarakimu iliyopigiwa mstari katika namba zifuatazo:
   (a) 64371 (b) 892161
   (c) 2464313 (d) 672314

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kulinganisha namba nzima

Namba nzima zinaweza kulinganishwa iwapo zipo sawa, kubwa kuliko au ndogo kuliko nyingine. Usawa wa namba huoneshwa kwa alama ( = ). Namba "kubwa kuliko" huoneshwa kwa alama ( > ) na namba "ndogo kuliko" huoneshwa kwa alama ( < ).

**Mfano**

Tumia alama <, = na > kulinganisha namba nzima hizi

(a) 8900 _____ 8090 (b) 3220 _____ 3220

(c) 3240 _____ 3420 (d) 715 _____ 517

**Jibu**

(a) 8900 > 8090 (b) 3220 = 3220

(c) 3240 < 3420 (d) 715 > 517

### Zoezi la 10

1. Tumia alama < , = na > kulinganisha namba zifuatazo. Swali 1(a) ni mfano.

(a) 12 < 21 (b) 15 ☐ 20 (c) 14 ☐ 7

(d) 20 ☐ 10 (e) 18 ☐ 13 (f) 19 ☐ 91

2. Tumia alama <, = na > kulinganisha namba zifuatazo.

(a) 2968 _____ 8962 (b) 972 _____ 972

(c) 3932 _____ 3239 (d) 999 _____ 1000

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(e) 8671 _____ 8761 (f) 5678 _____ 5678

(g) 9002 _____ 902 (h) 1000 _____ 100

3. Tony alipata alama 91, John alipata alama 78 na Emma alipata alama 85 katika mtihani wa Hisabati. Tumia alama ya ndogo kuliko (<) kulinganisha alama za Tony na John, kisha alama za John na Emma.

4. Jedwali lifuatalo linaonesha matunda mbalimbali na idadi yake.

| Aina ya matunda | Machungwa | Nanasi | Ndizi |
|---|---|---|---|
| Idadi ya matunda | 6851 | 1685 | 8516 |

Tumia alama <, > au = kulinganisha idadi ya matunda haya kama ifuatavyo:

(a) Machungwa ( _____ ) ndizi

(b) Machungwa ( _____ ) nanasi

(c) Ndizi ( _____ ) machungwa ( _____ ) nanasi


5. Baraka ana kadi yenye namba elfu tisa mia tano arobaini. Furaha ana kadi yenye namba 9450. Je, kati yao nani ana kadi yenye namba ndogo?

6. Halima ana kadi iliyoandikwa 2010. Kadi ya Yusufu imeandikwa 1577. Je, nani kati yao ana kadi iliyoandikwa namba kubwa?


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. Chunguza picha zifutazo, kisha jibu maswali yanayofuata:



Sanduku A



Sanduku B

(a) Je, kuna penseli ngapi kwenye sanduku A?

(b) Je, kuna penseli ngapi kwenye sanduku B?


(c) Je, ni sanduku gani lina idadi kubwa ya penseli kuliko lingine?

(d) Tumia alama =, < au > kulinganisha idadi ya penseli.


## Mfuatano katika namba nzima

Namba nzima zinaweza kupangwa kwa utaratibu maalumu. Mfululizo wa namba nzima unaozingatia mpangilio fulani au utaratibu maalumu hujulikana kama mfuatano katika namba nzima. Tunaweza kuchunguza na kutambua namba nzima inayofuata katika mfululizo wa namba nzima.


Chunguza idadi ya vizibo katika fungu A, B, na C.



Fungu A



Fungu B



Fungu C

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Fungu A lina vizibo 2, Fungu B lina vizibo 5. Fungu C lina vizibo 8. Namba ya idadi ya vizibo katika mafungu hayo zinaweza kuorodheshwa; 2, 5, 8. Kutoka Fungu A kwenda B vinaongezeka vizibo 3. Vilevile, kutoka Fungu B kwenda Fungu C vinaongezeka vizibo 3. Hii ina maana kwamba 2, 5, 8 ni mfuatano wa namba nzima. Iwapo utaunda fungu jingine kufuata utaratibu huo, fungu hilo litakuwa na vizibo 11. Yaani, 8 + 3 = 11. Mfuatano wa namba nzima utakuwa 2, 5, 8, 11.

## Mfano wa 1

Jaza namba nzima zinazofuata katika mfuatano wa namba zifuatazo: 1, 4, 7, 10, 13, 16, 19, ___, ___

**Njia**

Namba inayofuata inapatikana kwa kujumlisha 3 kwenye namba iliyotangulia.

1 + 3 = 4

4 + 3 = 7

7 + 3 = 10

10 + 3 = 13

13 + 3 = 16

16 + 3 = 19

19 + 3 = 22

22 + 3 = 25

Kwa hiyo, jibu ni 1, 4, 7, 10, 13, 16, 19, 22, 25.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 2

Jaza namba nzima zinazofuata katika mfuatano wa namba zifuatazo: 1, 3, 5, 7, 9, ___, ___

**Njia**

Namba nzima inayofuata inapatikana kwa kujumlisha 2 kwenye namba iliyotangulia.

1 + 2 = 3
3 + 2 = 5
5 + 2 = 7
7 + 2 = 9
9 + 2 = 11
11 + 2 = 13

Kwa hiyo, jibu ni 1, 3, 5, 7, 9, 11, 13.

## Mfano wa 3

Jaza namba nzima zinazofuata katika mfuatano wa namba hizi: 25, 23, 21, ___, ___

**Njia**

Namba nzima inayofuata katika mpangilio huu inapatikana kwa kutoa 2 kutoka namba iliyotangulia.

25 – 2 = 23
23 – 2 = 21
21 – 2 = 19
19 – 2 = 17

Kwa hiyo, jibu ni 25, 23, 21, 19, 17.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 4

Jaza namba nzima inayofuata katika mfuatano wa namba zifuatazo: 750, 600, 450, 300, 150, ___

**Njia**

Namba nzima inayofuata katika mpangilio huu inapatikana kwa kutoa 150 kutoka namba iliyotangulia.

750 – 150 = 600

600 – 150 = 450

450 – 150 = 300

300 – 150 = 150

150 – 150 = 0

Kwa hiyo, jibu ni 750, 600, 450, 300, 150, 0.

## Mfano wa 5

Jaza namba nzima inayokosekana katika mfuatano wa namba zifuatazo: 45, 41, 37, 33, ___

**Njia**

Namba nzima inayofuata katika mpangilio huu inapatikana kwa kutoa 4 kutoka namba iliyotangulia.

45 – 4 = 41

41 – 4 = 37

37 – 4 = 33

33 – 4 = 29

Kwa hiyo, jibu ni 45, 41, 37, 33, 29.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 11

1. Andika namba zilizopo kwenye jedwali kwa mpangilio unaofuatana kwa kuongezeka.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 22 | 7 | 15 | 14 | 10 |
| 11 | 28 | 18 | 20 | 24 |

7, ___, ___, ___, ___, ___, ___, ___, ___, ___

2. Andika namba zilizopo kwenye jedwali kwa mpangilio unaofuatana kwa kupungua.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 29 | 23 | 37 | 41 | 35 |
| 16 | 20 | 26 | 44 | 32 |

44, ___, ___, ___, ___, ___, ___, ___, ___, ___

3. Andika namba nzima zinazofuata kwa kila mfuatano:
   (a) 0, 2, 4, 6, ___, ___, ___
   (b) 11, 22, 33, 44, ___, ___, ___
   (c) 2, 6, 10, 14, 18, ___, ___, ___
   (d) 3, 8, 13, 18, 23, 28, 33, ___, ___, ___
   (e) 465, 466, 467, ___, ___, ___
   (f) 210, 220, 230, 240, 250, 260, ___, ___, ___

4. Andika namba nzima zinazofuata kwa kila mfuatano wa namba zifuatazo:
   (a) 14, 12, 10, 8, ___, ___, ___
   (b) 23, 20, 17, 14, 11, ___, ___
   (c) 56, 54, 52, ___, ___, ___
   (d) 69, 60, 51, 42, 33, ___, ___, ___
   (e) 95, 85, 75, 65, 55, 45, ___, ___, ___
   (f) 260, 250, 240, 230, 220, 210, ___, ___, ___

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Andika namba nzima zinazokosekana katika mifuatano ifuatayo:
   (a) 500, 600, _____, _____, 900, _____
   (b) 433, 430, _____, 424, _____, 418, 415, _____
   (c) 1027, 1023, _____, 1015, _____, 1007, _____
   (d) 4, 10, _____, 22, _____, 34, 40, 46, _____, 58
   (e) 415, 418, _____, 424, _____, 430, 433, _____
   (f) 1011, 1014, _____, 1020, 1023, _____, 1029

6. Chunguza namba nzima katika mifuatano uliyopewa katika jedwali lifuatalo kisha andika tendo lililotumika. Swali la 6(a) ni mfano.

| | **Mfuatano wa namba** | **Tendo lililotumika** |
|---|---|---|
| (a) | 1, 3, 5, 7, 9, 11, 13, 15, 17, 19 | Namba nzima kuongezeka kwa 2 katika kila hatua |
| (b) | 30, 25, 20, 15, 10, 5 | |
| (c) | 10, 20, 30, 40, 50, 60, 70 | |
| (d) | 500, 600, 700, 800 | |

7. Urefu wa milima minne ulirekodiwa kama ifuatavyo: Shira ulikuwa na meta 3626, Oldeani meta 3188, Meru meta 4566 na Klute meta 3952. Pangilia urefu wa milima kuanzia mlima mfupi zaidi hadi mrefu zaidi.

8. Majura aliuza vikombe 15 vya maziwa siku ya kwanza, aliendelea kuuza vikombe 8 zaidi ya siku iliyotangulia. Je, aliuza vikombe vingapi vya maziwa siku ya nne?

9. Kiwanda kilichapisha vitabu 50 siku ya kwanza. Vitabu viliongezeka 20 kila siku. Je,vitabu vingapi vilichapishwa siku ya tatu?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

10. Pamela alinunua maembe matatu siku ya kwanza, kisha aliendelea kununua maembe mawili zaidi ya siku iliyotangulia. Alinunua maembe mangapi siku ya nne?

11. Mkeya ana watoto watano.Tofauti ya umri kati ya kila watoto wawili wanaofuatana ni miaka minne. Ikiwa mtoto wa kwanza ana miaka 39, je mtoto wa mwisho ana umri gani?

## Kazi ya kufanya

Kujifunza namba nzima kwa njia ya masomo ya mtandaoni

### Maelezo

Tumia masomo ya mtandaoni kujifunza zaidi jinsi ya kusoma, kuandika, kutafuta thamani ya nafasi ya tarakimu, thamani ya tarakimu, kutengeneza mfuatano wa namba na kulinganisha namba nzima.

## Jikumbushe

1. Namba nzima huandikwa kwa namna mbili, yaani kwa numerali na kwa maneno
2. Katika kusoma namba nzima zingatia thamani ya nafasi na thamani ya tarakimu katika namba nzima
3. Alama za usawa (=), kubwa kuliko (>) na ndogo kuliko (<) zinatumiwa katika hisabati kuonesha uhusiano wa thamani kati ya vitu au namba nzima
4. Mfuatano wa namba nzima hufuata utaratibu maalumu
5. Ni muhimu kutambua tendo lililotumika kwa kila mfuatano wa namba nzima ili kupata mfuatano ulio sahihi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Msamiati | |
|---|---|
| Mfuatano | mfululizo wa vitu au namba unaozingatia utaratibu maalumu |
| Numerali | namba inayoandikwa kwa kutumia tarakimu |
| Tarakimu | namba kumi za mwanzo 0, 1, 2, 3, 4, 5, 6, 7, 8, na 9 |

## Zoezi la Marudio

1. Andika namba nzima inayotokana na thamani ya nafasi zifuatazo:
   (a) Maelfu saba, mamia sita, makumi mbili na mamoja mbili
   (b) Makumi elfu saba, maelfu sifuri, mamia sita, makumi nane na mamoja tatu
   (c) Makumi elfu mbili, maelfu tatu, mamia nne, makumi sita na mamoja sita
   (d) Mamia elfu nne, makumi elfu mbili, maelfu saba, mamia tatu, makumi moja na mamoja nne
   (e) Mamilioni moja, mamia elfu saba, makumi elfu nne, maelfu moja, mamia moja, makumi mbili na mamoja sifuri
   (f) Mamilioni tatu, mamia elfu saba, makumi elfu sita, maelfu tano, mamia tatu, makumi moja na mamoja tatu

2. Andika namba zifuatazo kwa kifupi.
   (a) 4000 + 200 + 50 + 1 =
   (b) 9000 + 800 + 30 + 3 =
   (c) 30000 + 3000 + 300 + 30 + 3 =

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) 600000 + 40000 + 4000 + 300 + 0 + 2 =

(e) 2000000 + 600000 + 40000 + 0 + 700 + 90 + 9 =

3. Jaza tarakimu ya namba nzima zifuatazo katika sehemu husika kwa kuzingatia thamani yake:

(a) 2063 ina maelfu ___, mamia___, makumi___na mamoja___.

(b) 8544 ina maelfu___, mamia___, makumi___na mamoja___.

(c) 3090 ina maelfu__, mamia___, makumi___ na mamoja___.

(d) 5713 ina maelfu___, mamia___, makumi___na mamoja___.

(e) 7226 ina maelfu___, mamia___ , makumi___na mamoja___.

4. Andika namba zifuatazo kwa numerali:

(a) Elfu moja na saba

(b) Elfu tano mia tano na tatu

(c) Elfu sita mia sita tisini na tisa

(d) Mia moja themanini elfu mia tano arobaini na moja

(e) Milioni mbili mia sita tisini na nane elfu mia sita hamsini na mbili

5. Andika namba zifuatazo kwa maneno:

(a) 2022 (b) 4969 (c) 8008

(d) 291649 (e) 1889 773

6. Fafanua namba zifuatazo:

(a) 7007 (b) 5712 (c) 9669

(d) 64645 (e) 303067


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. Panga namba zifuatazo kwa kuanza na namba ndogo hadi kubwa zaidi.
   (a) 5, 2, 6, 12, 19, 3, 1, 20,17
   (b) 36, 21, 15, 7, 10, 28, 45, 11
   (c) 789, 63, 32, 981, 252, 172, 426

8. Panga namba zifuatazo kwa mfuatano kuanza na namba kubwa hadi ndogo zaidi.
   (a) 125, 78, 111, 89, 305, 32, 120, 360, 115, 92, 412, 76, 61, 27, 56
   (b) 200, 903, 730, 341, 81, 199, 189, 800, 463, 72, 326, 247
   (c) 2500, 1 200, 5 000, 3 300, 4 500, 1 300, 6 000, 4600

9. Andika namba nzima inayowakilishwa katika kila abakasi:


   (a)





FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b)





(c)




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d)




10. Linganisha namba hizi kwa kutumia alama ya < , = au >.

(a) 8765 na 8576 (b) 2341 na 2341

(c) 2222 na 222 (d) 180541 na 180514

(e) 1234 na 2134 (f) 23466 na 24366

11. Jaza namba nzima zinazokosekana katika mifuatano ya namba zifuatazo:

(a) 71, 66, 61, 56, 51, 46, _____, _____, 31

(b) 100, 75, _____, 25, _____

(c) 100000, _____, 300000, 400000, _____

(d) 729600, 729590, _____, _____, _____, 729550

(e) 70, 61, 52, 43, 34, _____, _____, _____

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

12. Andika tendo lililotumika kupata mifuatano ya namba zifuatazo. Swali (a) ni mfano.

    (a) 1, 2, 3, 4, 5, 6, 7, 8 Kujumlisha moja kila hatua

    (b) 0, 4, 8, 12, 16, 20, 24, 28 _____

    (c) 68, 60, 52, 44, 36, 28, 20 _____

    (d) 100, 90, 80, 70, 60, 50, 40, 30, 20, 10, 0 _____

    (e) 1 444, 2 444, 3 444, 4 444, 5 444 _____

13. Jaza namba nzima zinazokosekana katika mipangilio ifuatayo:

    (a) 2398, 2390, 2382, _____, _____, 2358, 2350, _____

    (b) 52552, 51552, _____, _____, 48552, 47552, _____, 45552

    (c) _____, _____, _____, 840000, _____, 860000, ___

    (d) 2342, 2350, 2358, _____, _____, 2382, 2390, 2398, _____

    (e) 45562, 46562, _____, _____, 49562, 50562, _____, 52562

14. Mwalimu alipanga namba nzima katika mfuatano kama ifuatavyo: 45, 41, 37, 33, ___, ___. Tafuta namba mbili zilizofuata.

15. Namba nzima ya kwanza katika mfuatano ni 50. Iwapo 3 hupunguzwa katika kila hatua, namba nzima ya tano katika mfuatano itakuwa ngapi?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

16. Wanafunzi waliandika mfuatano wa namba nzima kwa kuanza na 3. Iwapo waliongeza 5 katika kila hatua, namba nzima ya sita katika mfuatano huo ilikuwa ngapi?

17. Andika mfuatano wa namba unaoruka 5 kwa kila hatua kuanzia 0 mpaka 50.

18. Andika mfuatano wa namba wenye tofauti ya 6 kwa kila hatua kuanzia 72 mpaka 0.

19. Mahudhurio ya wanafunzi wa darasa la tatu huongezeka kwa wanafunzi watatu kila wiki. Ikiwa wiki ya kwanza walikuwa 123, wiki ya nne walihudhuria wanafunzi wangapi?

20. Tumia namba 895674 kuandika:
    (a) thamani ya nafasi ya kila tarakimu.
    (b) thamani ya kila tarakimu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sura ya Pili

# Kujumlisha na kutoa namba nzima

**Utangulizi**

*Katika sura hii, utajifunza kujumlisha na kutoa namba nzima kwa ulalo na wima. Pia, utajifunza kufumbua mafumbo mbalimbali yenye dhana ya matendo ya kujumlisha na kutoa. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kupata jumla au tofauti ya idadi ya vitu mbalimbali.*

## Kujumlisha namba nzima

*Namba nzima zinaweza kujumlishwa bila kubadili au kwa kubadili kutegemeana na aina ya namba zinazojumlishwa.*

## Kujumlisha namba nzima bila kubadili

*Unapojumlisha namba nzima, hakikisha unazingatia thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba nzima. Anza kujumlisha mamoja, makumi, mamia, maelfu, makumi elfu, mamia elfu na kuendelea.*

### Kujumlisha namba nzima kwa ulalo

**Mfano wa 1**

3246 + 2312 =

**Njia**

*Panga namba kwa kufuata thamani ya kila tarakimu. Mpangilio huo ni kama ifuatavyo:*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


| Maelfu | Mamia | Makumi | Mamoja |
|---|---|---|---|
| 3 | 2 | 4 | 6 |

+

| Maelfu | Mamia | Makumi | Mamoja |
|---|---|---|---|
| 2 | 3 | 1 | 2 |

**Hatua**

1. Jumlisha mamoja na andika jibu katika nafasi ya mamoja.
2. Jumlisha makumi na andika jibu katika nafasi ya makumi.
3. Jumlisha mamia na andika jibu katika nafasi ya mamia.
4. Jumlisha maelfu na andika jibu katika nafasi ya maelfu.




Kwa hiyo, 3246 + 2312 = 5558.

## Mfano wa 2

68942 + 30051 =


**Hatua**

Jumlisha tarakimu kutoka kulia kuelekea kushoto.

1. Jumlisha mamoja: 2 + 1 = 3. Andika 3 katika nafasi ya mamoja.
2. Jumlisha makumi: 4 + 5 = 9. Andika 9 katika nafasi ya makumi.
3. Jumlisha mamia: 9 + 0 = 9. Andika 9 katika nafasi ya mamia.
4. Jumlisha maelfu: 8 + 0 = 8. Andika 8 katika nafasi ya maelfu.
5. Jumlisha makumi elfu: 6 + 3 = 9. Andika 9 katika nafasi ya makumi elfu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE





Kwa hiyo, 68942 + 30051 = 98993.

## Mfano wa 3

352411 + 136587 =

**Hatua**

1. Jumlisha mamoja na andika jibu katika nafasi ya mamoja.
2. Jumlisha makumi na andika jibu katika nafasi ya makumi.
3. Jumlisha mamia na andika jibu katika nafasi ya mamia.
4. Jumlisha maelfu na andika jibu katika nafasi ya maelfu.
5. Jumlisha makumi elfu na andika jibu katika nafasi ya makumi elfu.
6. Jumlisha mamia elfu na andika jibu katika nafasi ya mamia elfu.




Kwa hiyo, 352411 + 136587 = 488998.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

1. 4561 + 17 =
2. 9111 + 888 =
3. 705 + 1261 =
4. 2016 + 2161 =
5. 54622 + 44245 =
6. 53999 + 2000 =
7. 2141 + 42 =
8. 2411 + 136 =
9. 1418 + 2361 =
10. 6138 + 1 =
11. 631594 + 246305 =
12. 230000 + 144348 =
13. 80021 + 17734 =
14. 54622 + 44245 =
15. 54351 + 12045 =

### Kujumlisha namba nzima kwa wima

**Mfano wa 1**

$$\begin{array}{r} 6118 \\ +\ 1211 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia**

*Panga namba kwa kuzingatia thamani ya nafasi ya kila tarakimu, kisha fuata hatua zifuatazo:*

**Hatua**

1. *Jumlisha mamoja: 8 + 1 = 9. Andika 9 katika nafasi ya mamoja.*
2. *Jumlisha makumi: 1 + 1 = 2. Andika 2 katika nafasi ya makumi.*
3. *Jumlisha mamia: 1 + 2 = 3. Andika 3 katika nafasi ya mamia.*
4. *Jumlisha maelfu: 6 + 1 = 7. Andika 7 katika nafasi ya maelfu.*

   *Kwa hiyo, jibu ni 7329.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 2

$$\begin{array}{r} 45248 \\ +\ 20231 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia**

*Panga namba kwa kuzingatia thamani ya nafasi ya kila tarakimu, kisha fuata hatua zifuatazo:*

**Hatua**

1. *Jumlisha mamoja: 8 + 1 = 9. Andika 9 katika nafasi ya mamoja.*
2. *Jumlisha makumi: 4 + 3 = 7. Andika 7 katika nafasi ya makumi.*
3. *Jumlisha mamia: 2 + 2 = 4. Andika 4 katika nafasi ya mamia.*
4. *Jumlisha maelfu: 5 + 0 = 5. Andika 5 katika nafasi ya maelfu.*
5. *Jumlisha makumi elfu: 4 + 2 = 6. Andika 6 katika nafasi ya makumi elfu.*

   *Kwa hiyo, jibu ni 65 479.*

## Mfano wa 3

$$\begin{array}{r} 162792 \\ +\ 531203 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia**

*Panga namba kwa wima kama ifuatavyo:*

| | Mamia elfu | Makumi elfu | Maelfu | Mamia | Makumi | Mamoja |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 6 | 2 | 7 | 9 | 2 |
| + | 5 | 3 | 1 | 2 | 0 | 3 |
| | 6 | 9 | 3 | 9 | 9 | 5 |

*Kwa hiyo, jibu ni 693995.*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 4

```
  1222221
+  777777
--------
```

**Njia**

```
  1 222221
+   777777
---------
  1999998
```

## Zoezi la 2

1. 4612 + 1321 =

2. 3592 + 401 =

3. 2227 + 12 =

4. 2363 + 2111 =

5. 4350 + 5646 =

6. 82350 + 5213 =

7. 59261 + 40712 =

8. 84743 + 12251 =

9. 54721 + 33222 =

10. 818819 + 71110 =

11. 834532 + 154063 =

12. 140546 + 221121 =

13. 679448 + 110301 =

14. 789660 + 10118 =

15. 751210 + 12166 =

16. 323456 + 1676543 =

17. 1456317 + 333572 =

18. 999879 + 110 =

19. 751201 + 128780 =

20. 2013424 + 1976365 =

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kujumlisha namba nzima kwa kubadili

## Kujumlisha namba nzima kwa ulalo

### Mfano wa 1


6327 + 3496 =

**Njia**

Jumlisha tarakimu kuanzia kulia kuelekea kushoto.

**Hatua**

1. Jumlisha mamoja: 7 + 6 =13. Andika 3 katika nafasi ya mamoja. Badili mamoja 10 kuwa makumi 1. Peleka makumi 1 kwenye nafasi ya makumi.
2. Jumlisha makumi: 1 + 2 + 9 = 12. Andika 2 katika nafasi ya makumi. Badili makumi 10 kuwa mamia 1. Peleka mamia moja kwenye nafasi ya mamia.
3. Jumlisha mamia: 1 + 3 + 4 = 8. Andika 8 katika nafasi ya mamia.
4. Jumlisha maelfu: 6 + 3 = 9. Andika 9 katika nafasi ya maelfu.




Kwa hiyo, 6327 + 3496 = 9823.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 2


58271 + 32989 =

**Njia**

Jumlisha tarakimu kuanzia kulia kuelekea kushoto.

**Hatua**

1. Jumlisha mamoja: 1 + 9 = 10. Andika 0 katika nafasi ya mamoja. Badili mamoja 10 kuwa makumi 1. Peleka makumi 1 kwenye nafasi ya makumi.
2. Jumlisha makumi: 1 + 7 + 8 = 16. Andika 6 katika nafasi ya makumi. Badili makumi 10 kuwa mamia 1. Peleka mamia 1 kwenye nafasi ya mamia.
3. Jumlisha mamia: 1 + 2 + 9 =12. Andika 2 katika nafasi ya mamia. Badili mamia 10 kuwa maelfu 1. Peleka maelfu 1 kwenye nafasi ya maelfu.
4. Jumlisha maelfu:1 + 8 + 2 = 11. Andika 1 katika nafasi ya maelfu. Badili maelfu 10 kuwa makumi elfu 1.
   Peleka makumi elfu 1 kwenye nafasi ya makumi elfu.
5. Jumlisha makumi elfu: 1 + 5 + 3 = 9. Andika 9 katika nafasi ya makumi elfu.





Kwa hiyo, 58271 + 32989 = 91260.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 3

472395 + 134826 =

**Njia**




Kwa hiyo, 472395 + 134826 = 607221.

## Zoezi la 3

1. 7256 + 1796 =
2. 7531 + 1929 =
3. 8595 + 914 =
4. 3598 + 179 =
5. 4513 + 3299 =
6. 2643 + 993 =
7. 4951 + 1891 =
8. 7536 + 19 =
9. 768 + 7861 =
10. 7816 + 1832 =
11. 7576 + 817 =
12. 2619 + 1786 =
13. 1745 + 899 =
14. 1652 + 476 =
15. 15433 + 798 =
16. 53415 + 21045 =
17. 64124 + 16283 =
18. 75520 + 9221 =
19. 66612 + 24588 =
20. 162845 + 134027 =
21. 293586 + 26323 =
22. 567183 + 484921 =
23. 943573 + 56327 =
24. 720852 + 279168 =
25. 2964 + 298576 =

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kujumlisha namba nzima kwa wima

### Mfano wa 1

$$\begin{array}{r} 2361 \\ +\ 3899 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia**

Panga namba kwa wima kwa kuzingatia thamani ya nafasi ya kila tarakimu.

**Hatua**

| | |
|---|---|
| 1. Jumlisha mamoja: 1 + 9 = 10.<br>Andika 0 katika nafasi ya mamoja.<br>Badili mamoja 10 kuwa makumi 1.<br>Peleka makumi 1 kwenye nafasi ya makumi. | $\begin{array}{r} {\scriptstyle 1\ \ \ \ } \\ 2\,361 \\ +\ 3\,899 \\ \hline 0 \\ \hline \end{array}$ |
| 2. Jumlisha makumi: 1+ 6 + 9 = 16.<br>Andika 6 katika nafasi ya makumi.<br>Badili makumi 10 kuwa mamia 1.<br>Peleka mamia 1 kwenye nafasi ya mamia. | $\begin{array}{r} {\scriptstyle 1\ 1\ \ } \\ 2\,361 \\ +\ 3\,899 \\ \hline 60 \\ \hline \end{array}$ |
| 3. Jumlisha mamia: 1 + 3 + 8 = 12.<br>Andika 2 katika nafasi ya mamia.<br>Badili mamia 10 kuwa maelfu 1.<br>Peleka maelfu 1 kwenye nafasi ya maelfu. | $\begin{array}{r} {\scriptstyle 1\ 1\ 1\ } \\ 2\,361 \\ +\ 3\,899 \\ \hline 260 \\ \hline \end{array}$ |
| Jumlisha maelfu: 1 + 2 + 3 = 6. Andika 6 katika nafasi ya maelfu. | $\begin{array}{r} {\scriptstyle 1\ 1\ 1\ } \\ 2\,361 \\ +\ 3\,899 \\ \hline 6\,260 \\ \hline \end{array}$ |

Kwa hiyo, jibu ni 6260.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 2

$$\begin{array}{r} 228186 \\ +\ 374899 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Hatua**


1. Jumlisha mamoja: 6 + 9 = 15. Andika 5 katika nafasi ya mamoja. Badili mamoja 10 kuwa makumi 1. Peleka makumi 1 kwenye nafasi ya makumi.
2. Jumlisha makumi: 1 + 8 + 9 = 18. Andika 8 katika nafasi ya makumi. Badili makumi 10 kuwa mamia 1. Peleka mamia 1 kwenye nafasi ya mamia.
3. Jumlisha mamia: 1 + 1 + 8 = 10. Andika 0 katika nafasi ya mamia. Badili mamia 10 kuwa maelfu 1. Peleka maelfu 1 kwenye nafasi ya maelfu.
4. Jumlisha maelfu: 1 + 8 + 4 = 13. Andika 3 katika nafasi ya maelfu. Badili maelfu 10 kuwa makumi elfu1. Peleka makumi elfu 1 kwenye nafasi ya makumi elfu.
5. Jumlisha makumi elfu: 1 + 2 + 7 = 10. Andika 0 katika nafasi ya makumi elfu. Badili makumi elfu 10 kuwa mamia elfu 1. Peleka mamia elfu 1 kwenye nafasi ya mamia elfu.
6. Jumlisha mamia elfu: 1 + 2 + 3 = 6. Andika 6 katika nafasi ya mamia elfu.

Kwa hiyo, jibu ni 603085.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, kwa kutumia kadi ya namba unaweza kupanga namba hizo kama ifuatavyo:




Kwa hiyo, jibu ni 603085.

## Zoezi la 4

1. 6027 + 1784 = _____

2. 57336 + 12217 = _____

3. 48289 + 3457 = _____

4. 85519 + 2719 = _____

5. 856956 + 134689 = _____

6. 88456 + 154689 = _____

7. 489765 + 94538 = _____

8. 365284 + 476329 = _____

9. 624872 + 9341 = _____

10. 872146 + 34987 = _____

11. 167426 + 594 = _____

12. 877925 + 98 = _____

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

13. $100009 + 9991$

14. $89725 + 9999$

15. $80298 + 19712$

16. $998456 + 154689$

17. $6024872 + 3975127$

18. $8925778 + 7897987$

19. $1000009 + 999991$

20. $199001 + 950999$

21. *Chunguza njia walizotumia Ali, Rose na Dule kujumlisha 2792 na 1213. Tumia njia nyingine iliyo rahisi kwako kujumlisha namba hizo.*

| | |
|---|---|
| **Ali:** | 2792 + 1213 =<br>Jumlisha mamoja: 3 + 2 = 5.<br>Jumlisha makumi: 9 + 1 = 10.<br>Jumlisha mamia: 1 + 7 + 2 = 10.<br>Jumlisha maelfu: 1 + 2 + 1 = 4.<br>Kwa hiyo, 2792 + 1213 = 4005. |
| **Rose:** | 2792 + 1213 =<br>Alivunja namba hizo kama ifuatavyo:<br>2792 + 1213 = 2790 + 2 + 3 +1 210<br>= 2700 + 90 + 2 + 3 + 10 + 1200<br>= 2700 + 1200 + 90 + 2 + 3 + 10<br>= 3900 + 100 + 5 = 4005<br>Kwa hiyo, 2792 + 1213 = 4005. |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| **Dule:** | 2792 + 1213 =<br>Alifafanua namba hizo kama ifuatavyo:<br>2792 + 1213<br>= 2000 + 700 + 90 + 2 +1 000 + 200 + 10 + 3<br>= 2000 + 1000 + 700 + 200 + 90 + 10 + 2 + 3<br>= 3000 + 900 + 100 + 5 = 4005<br>Kwa hiyo, 2792 + 1213 = 4005. |
|---|---|

## Mafumbo yenye dhana ya kujumlisha namba nzima

### Mfano wa 1

Kiwanda cha kuchakata nyama kilinunua ng'ombe 137,527 mwaka juzi na ng'ombe 222,062 mwaka jana. Kiwanda hicho kilinunua ng'ombe wangapi kwa miaka yote miwili?

**Njia**

Idadi ya ng'ombe walionunuliwa mwaka juzi: 137527

Idadi ya ng'ombe walionunuliwa mwaka jana: + 222062

Jumla ya ng'ombe walionunuliwa kwa miaka yote miwili: 359589

Kwa hiyo, kiwanda kilinunua jumla ya ng'ombe 359,589 kwa miaka yote miwili.

### Mfano wa 2

Katika mbuga mojawapo ya wanyama nchini Tanzania, kuna pundamilia 78,696 na nyati 2,323. Je, kuna jumla ya wanyama wangapi katika mbuga hiyo?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Njia**

Idadi ya pundamilia: 78696
Idadi ya nyati: + 2323
Jumla ya wanyama: 81019

Kwa hiyo, jumla ya wanyama ni 81,019.

## Zoezi la 5

1. Kampuni mbili za uchapishaji zilizalisha vitabu kwa ajili ya shule za msingi. Kampuni ya kwanza ilitengeneza vitabu 5,900 na nyingine ilitengeneza vitabu 3,600. Je, kampuni hizo zilitengeneza jumla ya vitabu vingapi?
2. Mfugaji aliuza lita 35,752 za maziwa mwezi Januari. Katika mwezi Februari aliuza lita 27,888 za maziwa. Je, mfugaji aliuza jumla ya lita ngapi za maziwa kwa miezi hiyo miwili?
3. Mkulima ana miti ya mbao 1,982 na miti ya matunda 7,291. Je, mkulima huyo ana jumla ya miti mingapi?
4. Wagonjwa 4,618 wa malaria na 689 wa macho walitibiwa katika hospitali fulani. Je, jumla walitibiwa wagonjwa wangapi?
5. Mkulima alihifadhi kilogramu 25,677 za mahindi msimu wa kwanza wa mavuno. Akahifadhi tena kilogramu 21,913 za mahindi msimu wa pili wa mavuno. Je, mkulima alihifadhi jumla ya kilogramu ngapi za mahindi kwa misimu yote miwili?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Katika mwaka fulani, magari 9,436 yalikaguliwa mkoa wa Mtwara. Vilevile, katika mwaka huo huo, magari mengine 10,170 yalikaguliwa katika mkoa wa Ruvuma. Je, magari mangapi yalikaguliwa katika mikoa yote miwili kwa mwaka huo?

7. Shule ya Msingi Kakali ina madawati 2,588. Shule ya Msingi Dadawa ina madawati 8,813. Shule ya Msingi Rukuku ina madawati 10,554. Je, shule hizo zina jumla ya madawati mangapi?

8. Juma alivuna maembe 5,630 kutoka mti wa kwanza. Baadaye akavuna maembe 480 kutoka mti wa pili. Je, Juma alivuna jumla ya maembe mangapi?

9. Basi lilipakia matenga mawili ya machungwa.Tenga la kwanza lilikuwa na machungwa 2,376 na la pili lilikuwa na machungwa 4,638. Je, matenga hayo mawili yalikuwa na jumla ya machungwa mangapi?

10. Katika mkoa fulani, wanafunzi waliojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2015 ni 6,523. Mwaka 2016 walijiunga wanafunzi 7,212 na mwaka 2017 walijiunga wanafunzi 7,430. Je, jumla ya wanafunzi wangapi walijiunga kidato cha kwanza katika miaka hiyo mitatu?

## Kutoa namba nzima

Unapotoa namba nzima hakikisha unazingatia thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba. Anza kutoa mamoja, makumi, mamia na kuendelea.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutoa namba nzima bila kubadili


### Kutoa namba nzima kwa ulalo

**Mfano wa 1**

6874 – 2430 =

**Hatua**

1. Toa mamoja: 4 – 0 = 4. Andika 4 katika nafasi ya mamoja.
2. Toa makumi: 7 – 3 = 4. Andika 4 katika nafasi ya makumi.
3. Toa mamia: 8 – 4 = 4. Andika 4 katika nafasi ya mamia.
4. Toa maelfu: 6 – 2 = 4. Andika 4 katika nafasi ya maelfu.




Kwa hiyo, 6874 – 2430 = 4444.

**Mfano wa 2**


46781 – 1041 =

**Hatua**

1. Toa mamoja: 1 – 1 = 0. Andika 0 katika nafasi ya mamoja.
2. Toa makumi: 8 – 4 = 4. Andika 4 katika nafasi ya makumi.
3. Toa mamia: 7 – 0 = 7. Andika 7 katika nafasi ya mamia.
4. Toa maelfu: 6 – 1 = 5. Andika 5 katika nafasi ya maelfu.
5. Toa makumi elfu: 4 – 0 = 4. Andika 4 katika nafasi ya makumi elfu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




Kwa hiyo, 46781 – 1041 = 45740.

## Zoezi la 6

1. 9942 – 42 =
2. 4376 – 3245 =
3. 3760 – 2550 =
4. 3049 – 2017 =
5. 8973 – 7642 =
6. 4256 – 3132 =
7. 65458 – 21344 =
8. 87999 – 33422 =
9. 623440 – 2010 =
10. 568237 – 18113 =
11. 784969 – 543867 =
12. 987645 – 234 =
13. 2000652 – 331 =
14. 17897988 – 687888 =
15. 6999 456 – 2811222 =
16. 3334237 – 2223126 =
17. 9999999 – 7765555 =
18. 1079878 – 17561 =
19. 999789 – 347 =
20 1000005 – 2 =

## Kutoa namba nzima kwa wima

### Mfano wa 1

$$\begin{array}{r} 9854 \\ -\ 8743 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia**

*Panga namba nzima kwa kufuata thamani ya nafasi ya kila tarakimu katika namba. Mpangilio huo ni kama ulivyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | Maelfu | Mamia | Makumi | Mamoja |
|---|---|---|---|---|
| | 9 | 8 | 5 | 4 |
| – | 8 | 7 | 4 | 3 |
| | 1 | 1 | 1 | 1 |

Kwa hiyo, jibu ni 1111.

## Mfano wa 2

$$\begin{array}{r} 86597 \\ -\ 54326 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Hatua**

1. Toa mamoja: 7 – 6 =1. Andika 1 katika nafasi ya mamoja.
2. Toa makumi: 9 – 2 = 7. Andika 7 katika nafasi ya makumi.
3. Toa mamia: 5 – 3 = 2. Andika 2 katika nafasi ya mamia.
4. Toa maelfu: 6 – 4 = 2. Andika 2 katika nafasi ya maelfu.
5. Toa makumi elfu: 8 – 5 =3. Andika 3 katika nafasi ya makumi elfu.

   Kwa hiyo, jibu ni 32271.

## Mfano wa 3

$$\begin{array}{r} 984265 \\ -\ 632143 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia**

Hatua za kutoa kwa wima zinafanana na zile za ulalo. Anza kutoa mamoja, mamia hadi mamia elfu.

$$\begin{array}{r} 984265 \\ -\ 632143 \\ \hline 352122 \\ \hline \end{array}$$

Kwa hiyo, jibu ni 352122.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 7

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 7824 − 5612 | 2. | 4851 − 3720 | 3. | 4343 − 3231 |
| 4. | 8899 − 8768 | 5. | 6533 − 6322 | 6. | 7291 − 3231 |
| 7. | 69635 − 58313 | 8. | 75757 − 25252 | 9. | 99991 − 4340 |
| 10. | 237972 − 112451 | 11. | 823574 − 1230 | 12. | 912345 − 810212 |
| 13. | 695872 − 34751 | 14. | 987672 − 34521 | 15. | 652437 − 410316 |

## Kutoa namba nzima kwa kubadili

### Kutoa namba nzima kwa ulalo

**Mfano wa 1**

5371 – 3282 =

**Hatua**

1. *Toa mamoja: 1 – 2, 1 haitoshelezi kutoa 2. Chukua makumi 1 kutoka kwenye makumi 7, badili kuwa mamoja 10 kisha jumlisha na mamoja 1: 10 + 1 =11.*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hivyo, 11 – 2 = 9. Andika 9 katika nafasi ya mamoja. Kumbuka, kwenye makumi umechukua makumi 1. Hivyo, umebakiwa na makumi 6.

2. Toa makumi: 6 – 8, 6 haitoshelezi kutoa 8. Chukua mamia moja 1 kutoka kwenye mamia 3, badili kuwa makumi 10 kisha jumlisha na makumi 6: 10 + 6 = 16. Hivyo, 16 – 8 = 8. Andika 8 katika nafasi ya makumi. Kumbuka, kwenye mamia umechukua mamia 1. Hivyo, umebakiwa na mamia 2.
3. Toa mamia: 2 – 2 = 0. Andika 0 katika nafasi ya mamia.
4. Toa maelfu: 5 – 3 = 2. Andika 2 katika nafasi ya maelfu. Kwa hiyo, 5371 – 3282 = 2089.

## Mfano wa 2

982140 – 771671 =

**Hatua**

1. Toa mamoja: 0 – 1, 0 haitoshelezi kutoa 1. Chukua makumi 1 kutoka kwenye makumi 4, badili kuwa mamoja 10 kisha jumlisha na mamoja 0: 10 + 0 = 10. Hivyo, 10 – 1 = 9. Andika 9 katika nafasi ya mamoja. Kumbuka, kwenye makumi umechukua makumi 1. Hivyo, umebakiwa na makumi 3.
2. Toa makumi: 3 – 7, 3 haitoshelezi kutoa 7. Chukua mamia 1 kutoka kwenye mamia 1, badili kuwa makumi 10 kisha jumlisha na makumi 3: 10 + 3 = 13. Hivyo, 13 – 7 = 6. Andika 6 katika nafasi ya makumi. Kumbuka, kwenye mamia umechukua mamia 1. Hivyo, umebakiwa na mamia 0.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Toa mamia: 0 – 6, haitoshelezi. Chukua maelfu 1 kutoka kwenye maelfu 2, badili kuwa mamia 10 kisha jumlisha na mamia 0: 10 + 0 =10. Hivyo, 10 – 6 = 4. Andika 4 katika nafasi ya mamia. Kumbuka, kwenye maelfu umechukua maelfu 1. Hivyo, umebakiwa na maelfu 1.
4. Toa maelfu: 1 – 1 = 0. Andika 0 katika nafasi ya maelfu.
5. Toa makumi elfu: 8 – 7 = 1. Andika 1 katika nafasi ya makumi elfu.
6. Toa mamia elfu: 9 – 7 = 2. Andika 2 katika nafasi ya mamia elfu.

   Kwa hiyo, 982140 – 771671 = 210469.

## Zoezi la 8

1. 7100 – 4291=
2. 68721 – 6667 =
3. 6816 – 5824 =
4. 4133 – 2145 =
5. 65458 – 26344 =
6. 9026 – 3146 =
7. 7761 – 3872 =
8. 3465 – 1456 =
9. 84223 – 5843 =
10. 85446 – 2254 =
11. 44346 – 37016 =
12. 672354 – 51132 =
13. 976540 – 888666 =
14. 164945 – 99 =
15. 876124 – 697982 =

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutoa namba nzima kwa wima

### Mfano wa 1

$$\begin{array}{r} 6854 \\ -\ 3887 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

| **Hatua** | |
|---|---|
| Toa mamoja: 4 – 7, 4 haitoshelezi kutoa 7. Chukua makumi 1 kutoka kwenye makumi 5, badili kuwa makumi 10 kisha jumlisha na mamoja 4: 10 + 4 = 14. Hivyo, 14 – 7 = 7. Andika 7 katika nafasi ya mamoja. Kumbuka, kwenye makumi umechukua makumi 1. Hivyo, umebakiwa na makumi 4. | $\begin{array}{r} {\scriptstyle 4\,14} \\ 6\,\not{8}\not{5}\not{4} \\ -\ 3\,887 \\ \hline 7 \\ \hline \end{array}$ |
| Toa makumi: 4 – 8, 4 haitoshelezi kutoa 8. Chukua mamia 1 kwenye mamia 8, badili kuwa makumi 10 kisha jumlisha na makumi 4: 10 + 4 =14. Hivyo, 14 – 8 = 6. Andika 6 katika nafasi ya makumi. Kumbuka, kwenye mamia umechukua mamia 1. Hivyo, umebakiwa na mamia 7. | $\begin{array}{r} {\scriptstyle 14} \\ {\scriptstyle 7\not{1}4\,14} \\ 6\,\not{8}\not{5}\not{4} \\ -\ 3\,887 \\ \hline 67 \\ \hline \end{array}$ |
| Toa mamia: 7 – 8, 7 haitoshelezi kutoa 8. Chukua maelfu 1 kutoka kwenye maelfu 6, badili kuwa mamia 10 kisha jumlisha na mamia 7: 10 + 7 =17. Hivyo, 17 – 8 = 9. Andika 9 katika nafasi ya mamia. Kumbuka, kwenye maelfu umechukua maelfu 1. Hivyo, umebakiwa na maelfu 5. | $\begin{array}{r} {\scriptstyle 17\,14} \\ {\scriptstyle 5\not{7}\not{1}4\,14} \\ \not{6}\ \not{8}\not{5}\not{4} \\ -\ 3\,887 \\ \hline 967 \\ \hline \end{array}$ |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| Toa maelfu: 5 – 3 = 2. Andika 2 katika nafasi ya maelfu. | 1714<br>5714<br>~~6 854~~<br>−3 887<br>2 967 |

Kwa hiyo, jibu ni 2967.

## Mfano wa 2

$$\begin{array}{r} 87964 \\ -\ 49897 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia**

Hatua za kutoa kwa wima zinafanana na zile za mfano wa 1. Anza kutoa mamoja hadi makumi elfu.

$$\begin{array}{r} 87964 \\ -\ 49897 \\ \hline 38067 \\ \hline \end{array}$$

Kwa hiyo, jibu ni 38067.

## Zoezi la 9

1. $\begin{array}{r} 3822 \\ -\ 1713 \\ \hline \\ \hline \end{array}$

2. $\begin{array}{r} 1245 \\ -\ 158 \\ \hline \\ \hline \end{array}$

3. $\begin{array}{r} 45385 \\ -\ 34392 \\ \hline \\ \hline \end{array}$

4. $\begin{array}{r} 2083 \\ -\ 1976 \\ \hline \\ \hline \end{array}$

5. $\begin{array}{r} 30405 \\ -\ 1992 \\ \hline \\ \hline \end{array}$

6. $\begin{array}{r} 8433 \\ -\ 6377 \\ \hline \\ \hline \end{array}$

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. $3005 - 1992$

8. $64536 - 58323$

9. $55376 - 25445$

10. $873977 - 762582$

11. $682165 - 8987$

12. $875924 - 683678$

13. $600000 - 54164$

14. $87625 - 9734$

15. $666666 - 78947$

## Mafumbo yenye dhana ya kutoa namba nzima

### Mfano wa 1

Jumla ya ng'ombe na mbuzi katika wilaya fulani ni 2,139,500. Ikiwa ng'ombe ni 1,104,563, je wilaya hiyo ina mbuzi wangapi?

**Njia**

Jumla ya ng'ombe na mbuzi: 2139500

Idadi ya ng'ombe: $- \ 1104563$

Idadi ya mbuzi: 1034937

Kwa hiyo, wilaya ina mbuzi 1,034,937.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Mfano wa 2

Waoka mikate huoka mikate 72,324 kila siku. Siku moja walioka mikate 45458 tu. Je, mikate mingapi haikuokwa siku hiyo?

**Njia**

| | |
|---|---|
| Idadi ya mikate inayookwa kwa siku: | 72324 |
| Mikate iliyookwa siku hiyo: | – 45458 |
| Mikate ambayo haikuokwa siku hiyo: | 26866 |

Kwa hiyo, mikate ambayo haikuokwa siku hiyo ni 26,866.

## Zoezi la 10

1. Duka la Maria lina simu za mkononi na mezani 2,972. Ikiwa simu za mkononi ni 1,235, je, simu za mezani ni ngapi?
2. Muuza maembe alikuwa na maembe elfu nne mia tatu kumi na nane. Alimuuzia mfanyabiashara maembe elfu moja mia nne thelathini na tano. Je, alibakiwa na maembe mangapi?
3. Mvuvi alivua samaki elfu saba mia tatu themanini na moja. Aliuza samaki elfu tano mia saba tisini na mbili. Je, alibakiwa na samaki wangapi?
4. Remi alinunua matenga mawili yenye nyanya elfu sita mia nne arobaini. Nyanya elfu moja mia tatu na mbili zilikuwa zimeoza. Je, ni nyanya ngapi zilikuwa nzima?
5. Shule inahitaji madawati elfu tatu mia saba arobaini na tisa. Wazazi walichangia madawati elfu mbili mia tisa tisini na saba. Je, shule ina upungufu wa madawati mangapi?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Shule ilinunua madaftari elfu saba mia mbili hamsini na mbili. Juma na Tatu waliombwa kubeba madaftari hayo kuyapeleka stoo. Juma alibeba madaftari elfu tatu na thelathini na tisa. Je, Tatu alibeba madaftari mangapi?
7. Katika mwaka fulani wanafunzi walipanda miti elfu tatu mia nne themanini. Baada ya miaka miwili, miti mia tano themanini na saba ilikauka. Je, miti mingapi ilibaki kipindi hicho?
8. Chama cha ushirika kilifyatua matofali 287,891 kati ya mahitaji ya matofali 482,674. Ni matofali mangapi hayakufyatuliwa?
9. Fundi alilipwa shilingi 845,750 kwa ujenzi wa choo cha shule. Gharama za ufundi zilikuwa shilingi 974,500. Je, zilipungua shilingi ngapi kukamilisha malipo yake?
10. Kata fulani ina wapiga kura elfu sita mia nane sabini na nne. Wapiga kura elfu tatu na themanini na saba walijitokeza kupiga kura. Je, ni wapiga kura wangapi hawakujitokeza kupiga kura?
11. Kampuni moja iliagizwa kuleta shuleni mabati elfu mbili mia nane na saba. Kampuni hiyo ilileta mabati elfu mbili mia tatu tisini na nane. Je, mabati mangapi hayakuletwa?
12. Kulwa alivuna magunia elfu tano na arobaini na saba ya maharage mwaka wa kwanza. Pia, alivuna magunia elfu tatu mia nne thelathini na nane ya maharage mwaka wa pili. Je, mwaka wa pili alivuna magunia mangapi pungufu ukilinganisha na mwaka wa kwanza?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya

Kujifunza zaidi kubaini matendo ya kujumlisha na kutoa namba nzima kwa njia ya masomo ya mtandaoni

### Maelezo

Chunguza mifano mbalimbali ya kujumlisha na kutoa namba nzima kwa njia ya masomo ya mtandaoni.

### Jikumbushe

1. Unapojumlisha au kutoa namba nzima, panga tarakimu kwa wima au ulalo. Anza kujumlisha au kutoa mamoja, makumi, mamia, maelfu, makumi elfu, mamia elfu na kuendelea

2. Unapofumbua mafumbo:
   (a) Tafsiri maelezo kupata tendo litakalotumika
   (b) Chambua maelezo kupata hesabu inayohusika
   (c) Baada ya kukokotoa, rejea swali na jibu swali kwa maneno

## Zoezi la marudio

1. $6142 + 4226$

2. $8937 - 27$

3. $55394 + 1295$

4. $47326 - 32198$

5. $2696 + 2398$

6. $638345 - 225221$

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. $\begin{array}{r} 55394 \\ +\ 1295 \\ \hline \\ \hline \end{array}$

8. $\begin{array}{r} 7623 \\ -\ 278 \\ \hline \\ \hline \end{array}$

9. $6145 + 312 =$

10. $8912 + 88 =$

11. $54273 + 12632 =$

12 $76832 + 2126 =$

13. $9051 - 4030 =$

14. $4177 - 408 =$

15. $548123 - 253700 =$

16. $59635 - 926 =$

17. Salum anahitaji matofali elfu nne na mia tano sabini kujenga nyumba yake. Kwa sasa anayo matofali elfu moja mia mbili sabini. Je, anahitaji kuongeza matofali mangapi zaidi ili kujenga nyumba yake?

18. Wananchi wa Tabora waliotesha miti elfu tisa mia tisa tisini katika miaka miwili. Ikiwa mwaka wa kwanza wataotesha miti elfu tano na sabini, je mwaka wa pili waliotesha miti mingapi?

19. Mwalimu Mponela alikuwa na madaftari 7,568. Ikiwa aliwapatia wanafunzi wake madaftari 5,368, je alibakiwa na madaftari mangapi?

20. Shule ina jumla ya wanafunzi 3,270. Kati yao wasichana ni 1,560. Je, shule hiyo ina wavulana wangapi?

21. Kata moja ina wakazi 6,328 na kata nyingine ina wakazi 2,590. Je, kata zote mbili zina jumla ya wakazi wangapi?

22. John anafuga kuku 4,569 na Ashura anafuga kuku 5,200. Je, wote kwa pamoja wana jumla ya kuku wangapi?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sura ya Tatu

# Vipimo vya urefu, uzani na ujazo

**Utangulizi**

*Katika sura hii utajifunza vipimo vya urefu, uzani na ujazo. Utaweza kukadiria na kulinganisha urefu, uzani na ujazo wa vitu mbalimbali. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kupima urefu, uzani na ujazo na kutumia vitu kulingana na mahitaji.*

## Vipimo vya urefu


*Urefu ni umbali kutoka sehemu moja hadi nyingine. Urefu unaweza kupimwa kwa kutumia vipimio visivyo rasmi na vipimio rasmi vya urefu.*

## Vipimio visivyo rasmi vya urefu

*Vipimio visivyo rasmi hutumiwa kulingana na aina ya vitu vinavyopimwa. Mfano kupima urefu wa ubao au meza unaweza kutumia vipimio visivyo rasmi kama vile hatua za miguu, fimbo, kamba na kiganja cha mkono. Vipimio hivyo visivyo rasmi hutoa majibu yasiyofanana kila vinapotumika. Sababu ya kutofautiana ni kwamba urefu wa kitu utategemea urefu wa kiganja cha mkono. Watu wawili wenye urefu tofauti wa viganja vya mikono hutoa majibu tofauti. Picha ifuatayo inaonesha mwanafunzi akipima urefu wa meza kwa kutumia kiganja cha mkono.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kazi ya kufanya 1:** Kupima urefu wa darasa

1. Pima urefu wa darasa kwa kutumia hatua za miguu.
2. Rekodi urefu wa darasa.
3. Mwambie mwenzako naye apime na kurekodi urefu wa darasa kwa kutumia hatua za miguu.
4. Linganisha hatua za miguu zilizorekodiwa kutoka 2 na 3.
5. Je, idadi ya hatua mlizopima zinatofautiana? Eleza sababu ya jibu lako.


## Vipimio rasmi vya urefu

Vipimio rasmi vya urefu vinakubalika na vinatoa majibu yanayofanana mahali popote vinapotumika. Vipimio hivyo ni pamoja na rula na futikamba. Vipimio hivi hupima urefu katika vipimo kama vile milimeta (mm), sentimeta (sm), meta (m) na kilometa (km).


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Picha ifuatayo inaonesha baadhi ya vipimio rasmi vya urefu.




Rula



Futikamba mbalimbali

## **Kazi ya kufanya 2:** Kupima urefu wa vitu mbalimbali

1. Bainisha vitu mbalimbali vinavyoweza kupimwa kwa vipimio rasmi na visivyo rasmi.
2. Pima na kurekodi urefu wa kitu kimoja kwa vipimio rasmi na visivyo rasmi.
3. Rekodi matokeo ya vipimo vilivyopatikana kwa kutumia vipimo rasmi na visivyo rasmi. Je, vipimo hivyo vinalingana vipi?

## **Kazi ya kufanya 3:** Kupima urefu wa daftari

1. Pima urefu wa daftari lako kwa kutumia rula yenye kipimo cha sentimeta.
2. Rekodi urefu ulioupata katika hatua ya 1.
3. Rudia hatua ya 1 kwa kutumia futikamba.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


4. Rekodi urefu uliopata kwa sentimeta katika hatua ya 3.
5. Linganisha vipimo ulivyopata katika hatua ya 3 na 4.
6. Eleza ulichogundua katika hatua ya 5.

## Vipimo vya milimeta na sentimeta

Vipimo vya milimeta na sentimeta hutumika mara nyingi tunapopima vitu kwa kutumia rula. Rula hupima urefu katika sentimeta na milimeta. Sentimeta moja ni sawa na milimeta 10. Kipimo kidogo cha rula ni milimeta.

### Mfano wa 1

Kipande cha kitambaa kilichopimwa katika picha ifuatayo kina urefu gani?





**Jibu**

Urefu wa kipande cha kitambaa ni sm 5.

### Mfano wa 2

Kipande cha ubao kilichopimwa katika picha ifuatayo kina urefu gani?




**Jibu**

Urefu wa kipande cha ubao ni sm 3 na mm 5.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Zoezi la 1

Pima na rekodi urefu wa vitu vifuatavyo katika sm na mm:

1. Meza
2. Dawati
3. Kalamu
4. Daftari
5. Rula
6. Kitabu
7. Ufutio
8. Mkebe

### Kipimo cha meta

Kipimo cha meta ni cha msingi katika kupima urefu. Kipimo hiki hutumika kupima vitu kama vile urefu wa chumba cha darasa. Urefu wa meta moja ni sawa na sentimeta 100, au kwa kifupi ni m1 = sm 100. Mchoro ufuatao unaonesha rula yenye urefu wa sentimeta 100 au meta moja.




## Kazi ya kufanya 4: Kupima urefu wa vitu katika meta

1. Pima vitu vifuatavyo katika meta na sentimeta.

| | Kitu | Urefu |
|---|---|---|
| (a) | Meza ya mwalimu | |
| (b) | Mlango wa darasa | |
| (c) | Dawati | |

2. Rekodi urefu wa kila kitu ulichopima.
3. Je, ni kitu gani kirefu kuliko vyote? Andika thamani yake.

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kipimo cha kilometa**

*Kipimo cha kilometa hutumika katika kupima urefu mkubwa zaidi. Hii ni pamoja na umbali wa sehemu mbili zilizo mbali Kwa mfano, umbali kutoka mji mmoja hadi mwingine hupimwa kwa kilometa.Umbali wa kilometa moja ni sawa na meta elfu moja. Kwa kifupi km 1 = m 1000.*

## Zoezi la 2

1. *Utatumia kipimo gani kati ya sm, m, na km kupima vitu vifuatavyo?*
   - *(a) Urefu wako*
   - *(b) Umbali kutoka darasa hadi choo cha shule*
   - *(c) Umbali kutoka nyumbani hadi shuleni*
   - *(d) Urefu wa kipande cha chaki*
2. *Amina alipima ubao kwa kutumia rula. John alipima ubao huohuo kwa kutumia kiganja cha mkono. Je, ni nani aliyepata jibu lenye usahihi zaidi? Eleza sababu ya jibu lako?*
3. *Umbali kutoka shuleni hadi zahanati ni m 800. Umbali kutoka shule hiyo hadi sokoni ni km 1. Kati ya zahanati na sokoni, wapi ni mbali zaidi kutoka shuleni?*
4. *Andika urefu wa kalamu katika mchoro huu.*




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vipimo vya uzani

*Uzani ni kipimo cha uzito wa vitu. Uzani wa kitu unaweza kupimwa kwa kutumia vipimio rasmi na visivyo rasmi vya uzani.*

## Vipimio visivyo rasmi vya uzani

*Vipimo visivyo rasmi vya uzani ni kama vikombe, vijiko, debe, magunia, ndoo na makasha. Picha ifuatayo inaonesha ndoo mbili zenye mchele.*



Ndoo A





Ndoo B

*Je, ni ndoo ipi ina uzani mkubwa wa mchele? Eleza sababu ya jibu lako.*

## Vipimio rasmi vya uzani

*Vipimio rasmi vya uzani wa vitu mbalimbali ni mizani. Vipimio hivyo hutambulika kitaifa na kimataifa. Picha zifuatazo zinaonesha baadhi ya mizani.*







FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kilogramu na gramu

*Uzani wa vitu mbalimbali hurekodiwa mara kwa mara kwa kutumia vipimo vya gramu na kilogramu. Kipimo cha gramu ni kidogo kuliko kilogramu. Uhusiano wa kilogramu na gramu ni kama ifuatavyo:*

Kilogramu (kg) 1 = gramu (g) 1 000

Nusu kilogramu = gramu 500

Robo kilogramu = gramu 250

**Kazi ya kufanya 5:** Kupima uzani wa vitu katika gramu na kilogramu

1. Andaa vitu mbalimbali katika mazingira yako vinavyoweza kupimwa kwa uzani.
2. Chagua vitu viwili na pima uzani wake.
3. Pima kiasi cha gramu 750 za kitu cha kwanza, kisha pima kilogramu moja ya kitu cha pili.
4. Kati ya vitu viwili ulivyopima, kipi ni kizito kuliko kingine?

## Zoezi la 3

1. Kipimo kipi kati ya gramu na kilogramu kinaweza kutumika kupima vitu vifuatavyo?
   (a) Uzani wa kitabu cha Hisabati
   (b) Gunia la mchele
   (c) Nyama
   (d) Uzani wa mwanafunzi
   (e) Begi la madaftari
   (f) Kipande cha chaki

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Pima uzani wa vitu vifuatavyo:
   (a) Chupa tupu ya soda
   (b) Daftari
   (c) Mkebe wa vifaa vya kihisabati

3. Katika vitu ulivyopima katika swali la pili:
   (a) Kipi kina uzani mdogo zaidi?
   (b) Kipi kina uzani mkubwa zaidi?

4. Orodhesha vitu vingine vitano vinavyopimwa kwa kutumia vipimio rasmi vya uzani.

5. Panga vipimo vifuatavyo kutoka uzani mkubwa kwenda mdogo: g 1600, g 500, kg 250, kg 155 na g 650.

6. Zipora anasema uzani wa gramu 1,000 ni mkubwa kuliko ule wa kilogramu moja. Je, Zipora yuko sahihi? Eleza jibu lako.

## Vipimo vya ujazo

Ujazo ni kiasi cha nafasi kinachochukuliwa na kitu. Ujazo unaweza kupimwa kwa kutumia vipimio rasmi na visivyo rasmi.

## Vipimio visivyo rasmi vya ujazo

Vipimio visivyo rasmi vya ujazo ni kama vijiko, vikombe na ndoo. Picha ifuatayo inaonesha wanafunzi wanapima ujazo wa maji kwa kutumia vikombe na ndoo.

Wanafunzi wanajaza maji katika ndoo mbili zilizo sawa. Kila mtoto anajaza ndoo yake kwa kutumia kikombe. Watoto hao wamejaza idadi sawa za vikombe vya maji katika ndoo zao.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Je, ndoo hizo zitakuwa na kiwango sawa cha maji? Eleza sababu ya jibu lako.



**Kazi ya kufanya 6:** Kupima ujazo wa maji




1. Andaa vyombo viwili vya ujazo vilivyo sawa.
2. Jaza maji katika vyombo hivyo ukihesabu idadi ya vikombe.
3. Mwambie rafiki yako ajaze maji katika vyombo hivyo hivyo akihesabu idadi ya vikombe pia.
4. Rekodi idadi ya vikombe vilivyotumika kujaza chombo chako na cha rafiki yako.
5. Je, idadi ya vikombe vilivyojaza vyombo vinatofautiana? Eleza sababu ya jibu lako.
6. Bainisha vitu vingine vitatu katika mazingira yako unavyoweza kupima.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vipimio rasmi vya ujazo

Vipimio rasmi vya ujazo havitofautiani katika kutoa majibu mahali popote vinapotumika. Vipimio hivyo ni kama bika, silinda kipimo na chupa yenye vipimo.

Picha zifuatazo zinaonesha baadhi ya vipimio rasmi vya ujazo

| Kipimio | Jina |
|---|---|
|   | bika |
|   | silinda kipimo |
|   | chupa yenye vipimo |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Vipimo vya lita na mililita

Vipimo vya ujazo vinavyotumika mara kwa mara ni lita (L) na mililita(mL). Kipimo cha mililita ni kidogo kuliko lita. Vipimo vyote hivyo hutumika kupima ujazo. Uhusiano wa lita na mililita ni kama ifuatavyo:

Lita (L) 1 = mililita (mL) 1000

Nusu lita = mililita 500

Robo lita = mililita 250

**Kazi ya kufanya 7:** Kupima ujazo wa maji

1. Andaa silinda za kupimia.
2. Jaza maji kwenye silinda mpaka nusu ya ujazo wake.
3. Soma ujazo wake.

## Zoezi la 4

1. Panga vipimo vifuatavyo kuanzia kipimo kidogo kwenda kikubwa; mL 450, mL 40, L 2 na mL 4.


2. Chunguza jedwali lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata:


| Jagi | Lita | Chupa | Mizani msawazo |
|---|---|---|---|
| Rula ndefu | Boksi | Bomba la sindano | Ndoo |

   (a) Vipimio vipi vinatumika kupima ujazo?
   (b) Kipimo kipi kinapima ujazo?
   (c) Orodhesha vipimio vinavyopima ujazo mkubwa.
   (d) Orodhesha vipimio vinavyopima ujazo mdogo.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Chunguza vipimio vifuatavyo kisha andika kiasi kilichopo kwenye kila kipimio.

(a) 


(b) 


4. Ng'ombe hutoa lita 20 za maziwa kila siku. Hutoa lita ngapi za maziwa kwa siku tatu?

5. Faraja alinunua sharubati yenye ujazo wa lita moja. Kisha akamimina mL 500 kwenye chupa na kumpa rafiki yake. Je, Faraja alibakiwa na kiasi gani cha sharubati?

## Kazi ya kufanya 8: Chunguza vipimio mbalimbali katika maisha ya kila siku

1. Tembelea duka lililokaribu yako linalouza vitu mbalimbali.
2. Bainisha jinsi wanavyopima urefu, uzani na ujazo.
3. Bainisha vitu vitatu kati ya vyote ulivyoviona.
4. Je, vitu gani hutumika kupima urefu, uzani na ujazo katika vitu ulivyovibainisha katika hatua ya 3?
5. Rekodi urefu, uzani na ujazo wa vitu ulivyovibainisha.

## Kazi ya kufanya 9

Kujifunza zaidi vipimo vya urefu, uzani na ujazo kwa njia ya masomo ya mtandaoni

### Maelezo

Tumia masomo ya mtandaoni kujifunza zaidi juu ya vipimo vya urefu, uzani na ujazo katika masomo ya mtandaoni.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Jikumbushe

1. Kipimo cha msingi cha urefu ni meta (m)
2. Kipimo cha msingi cha uzani ni gramu (g)
3. Kipimo cha msingi cha ujazo ni lita (L)
4. Uhusiano wa meta na sentimeta ni m 1 = sm 100
5. Uhusiano wa kilogramu na gramu ni kg 1 = g 1000
6. Uhusiano wa lita na mililita ni L 1 = mL 1000

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Urefu | Umbali kutoka sehemu moja hadi nyingine. |
| Kipimio | namba inayoandikwa kwa kutumia tarakimu |
| Uzani | Uzito wa kitu. |
| Ujazo | Kiasi cha nafasi kilichochukuliwa na kitu. |

## Zoezi la Marudio

1. Chagua kipimo kinachoweza kuwa sahihi kutoka fungu B kupima urefu katika fungu A.

**Fungu A**

(a) Urefu wa ofisi ya walimu _____

(b) Urefu wa kipande cha chaki _____

(c) Urefu wa barabara kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam ni _____


**Fungu B**

| | | |
|---|---|---|
| Meta (m) | Sentimeta (sm) | Kilometa (km) |
| Kilogramu (kg) | Mililita(mL) | Lita(L) |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Kipi kati ya bidhaa zifuatazo kinaweza kukadiriwa kuwa na uzani wa kilogramu moja?
   (a) Baiskeli
   (b) nanasi
   (c) kipande cha karatasi

3. Katika picha zifuatazo andika vipimo vya uzani unaoweza kukadiria kati ya kilogramu au gramu. Swali (a) ni mfano

| | **Picha** | **Uzani unakadiriwa katika gramu au kilogramu** |
|---|---|---|
| (a) |  Yai | Gramu |
| (b) |  Kizibo | _____ |
| (c) |  Ng'ombe | _____ |
| (d) |  Penseli | _____ |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Iwapo mawe mawili yenye uzani wa g 500 na g 250 yalitumika kulinganisha uzani wa mchele. Je,mchele una uzani gani?
5. Umepewa mawe mawili yenye uzani wa g 250 na moja lenye uzani wa g 500. Je, utafanyaje kupima kilogramu moja?
6. Iwapo umepewa vipimio vyenye ujazo wa mL 150, mL 400 na mL 500. Je, utatumia vipimio gani kupima mililita 550?
7. Mzee Kinene amebakiwa na dawa ya ng'ombe ya mL 750 kwenye chupa ya mL 1000. Je, anahitaji mililita ngapi ili aweze kujaza chupa hiyo ya dawa?
8. Mlonganile alinunua chupa ya maji ya lita moja. Iwapo alikunywa mL 500 wakati wa chakula, je alibakiwa na kiasi gani cha maji?
9. Aisha aliambiwa apime urefu wa uwanja wa mpira wa pete. Kipi kati ya vipimo vifuatavyo kinafaa zaidi kuwakilisha umbali huu: sm, m au km? Eleza sababu ya jibu lako.
10. Rula ya Kamene imevunjika na inaanzia katika alama ya sm 3. Kamene anataka kuchora kipande cha mstari wenye urefu wa sm 5. Je, ataishia kwenye alama ipi kwenye rula hiyo?
11. Utatumia kipimo gani kati ya gramu na kilogramu kupima uzani wa chungwa?
12. Ikiwa gunia la viazi lina uzani wa g 2000 na gunia la mchele lina uzani wa kg 1. Je, ni gunia gani lenye uzani mkubwa kuliko lingine?
13. Clara alinunua mafuta ya kupikia yenye ujazo wa mL 500. Alitumia mafuta yenye ujazo wa mL 250. Je, alibakiwa na mafuta ya ujazo wa kiasi gani?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sura ya Nne

# Maumbo

**Utangulizi**

*Katika sura hii utajifunza maumbo ya aina mbalimbali. Utajifunza nukta, mstari, kipande cha mstari na mwale. Utajifunza kuunda maumbo bapa kwa kutumia nukta, mstari na kipande cha mstari. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia maumbo katika shughuli mbalimbali kama vile upishi, ushoni, ujenzi, useremala, uchoraji na utengenezaji wa vitu mbalimbali.*

## Nukta, mstari, kipande cha mstari na mwale

*Nukta, mstari, kipande cha mstari na mwale ni maumbo ya msingi katika uhusiano wa maumbo mbalimbali.*

### Nukta

*Nukta ni umbo ambalo halina ukubwa linaloonesha mahali. Nukta haina urefu wala upana na huwakilishwa na herufi kubwa. Ifuatayo ni mifano inayoonesha nukta A, B na C.*




*Katika mifano hii, nukta A, B, na C zinaonesha mahali tofauti.*

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya 1:** Kuonesha mahali kwa kutumia nukta

1. Tumia penseli kuweka nukta tano tofauti kwenye karatasi.
2. Andika majina ya nukta hizo kwa kutumia herufi kubwa.

**Mstari**

Mstari huundwa na seti ya nukta zilizounganishwa pamoja na kuendelezwa pande mbili tofauti bila kuwa na mwisho. Mara nyingi mstari huoneshwa kwa kutumia mstari mnyoofu ambao huwekewa alama ya ⟷ kila upande ili kuonesha kuwa hauna mwisho. Mstari huweza kuoneshwa kwa kutumia nukta mbili zilizopo kwenye huo mstari. Kielelezo kifuatacho ni mifano ya mistari minyoofu.





Kwa hiyo, $\overleftrightarrow{EF}$ au $\overleftrightarrow{EF}$ ni kifupi cha mstari mnyoofu EF au FE. Vilevile, $\overleftrightarrow{AB}$ au $\overleftrightarrow{BA}$ na $\overleftrightarrow{CD}$ au $\overleftrightarrow{DC}$ ni mistari minyoofu.

**Mfano**

Chora mstari, kisha weka nukta A na B zenye umbali wa sm 10 kutoka nukta A hadi nukta B.

**Jibu**

Mstari wenye nukta A na B zenye umbali wa sm10 kutoka nukta A hadi B.




FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kipande cha mstari**


Kipande cha mstari ni mstari mnyoofu unaounganisha nukta mbili tofauti. Kipande cha mstari kinaweza kupimwa urefu wake kupitia umbali uliopo kati ya nukta mbili za mwisho. Kipande cha mstari kinachounganisha nukta A na B huandikwa $\overline{AB}$ au $\overline{BA}$.

**Kazi ya kufanya 2:** Kuchora kipande cha mstari

1. Unganisha nukta A na B, C na D, na E na F kwa kutumia penseli bila rula.




2. Unganisha nukta A na B, C na D, na E na F kwa kutumia penseli na rula





3. Umegundua nini katika hatua ya 1 na ya 2?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Ni katika kazi ipi mistari ifuatayo imetengenezwa?




**Sifa za kipande cha mstari**

Kipande cha mstari kina sifa zifuatazo:


(a) Kimenyooka

(b) Hakina unene

(c) Kina mwanzo katika nukta moja na mwisho kwenye nukta nyingine

**Mfano wa 1**

Katika michoro ifuatayo bainisha mstari, kipande cha mstari au siyo mstari wala kipande cha mstari.




**Jibu**

(a) Ni mstari kwa sababu hauna nukta ya mwisho katika pande zote mbili.

(b) Ni kipande cha mstari kwa sababu kina pande mbili zenye nukta mwishoni.


(c) Si kipande cha mstari kwa sababu ina upande unaoanza na nukta na upande mmoja umewekewa mshale.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Mfano wa 2

Andika jina la kila kipande cha mstari katika michoro ifuatayo:

(a)




(b)




(c)





**Jibu**

(a) $\overline{DQ}$ (b) $\overline{CD}$ (c) $\overline{AB}$

## Mfano wa 3

Andika vipande vyote vya mstari kutoka kwenye mchoro ufuatao:





**Jibu**

$\overline{AB}$, $\overline{AC}$, $\overline{AD}$, $\overline{BC}$, $\overline{BD}$ na $\overline{CD}$

## Mfano wa 4

Kuna vipande vingapi vya mstari katika mchoro ufuatao:



**Jibu**

Kuna vipande 8 vya mistari.

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

1. Chora vipande vya mistari vyenye urefu ufuatao:
   (a) $\overline{PQ}$ = sm 4 (b) $\overline{CD}$ = sm 5
   (c) $\overline{LM}$ = sm 6 (d) $\overline{JK}$ = sm 7
   (e) $\overline{XY}$ = sm 8 (f) $\overline{EF}$ = sm 9
   (g) $\overline{MN}$ = sm 10
2. Umbo mraba lina vipande vya mstari vingapi?
3. Kipi kati ya vifuatavyo kina wakilisha kipande cha mstari?
   (a) $\overrightarrow{AB}$ (b) $\overleftrightarrow{AB}$ (c) $\overleftarrow{AB}$ (d) $\overline{AB}$
4. Ipi ni mifano ya vipande vya mistari katika maisha yetu ya kila siku?

### Mwale

Mwale ni kipande cha mstari kinachoendelezwa upande mmoja bila kikomo. Upande unaoendelea bila kikomo huwekewa mshale. Mifano ya miale ni kama inavyooneshwa katika kielelezo kifuatacho:




Mwale huandikwa na alama $\longrightarrow$ inayowakilisha mwale. Kwa mfano mwale AB huandikwa $\overrightarrow{AB}$ na mwale BA huandikwa $\overrightarrow{BA}$.

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya 3:** Kuchora mwale

1. Tumia rula kuchora kipande cha mstari AB.
2. Endeleza kipande cha mstari AB upande wa kushoto au kulia, kisha kiwekee mshale kuonesha uelekeo.
3. Rudia hatua ya 1 na 2 kuchora miale mitatu, kisha andika majina yake.

## Mfano wa 1

Katika mchoro ufuatao ipi ni nukta ya mwisho wa mwale AC?





**Jibu**

Kwa kuwa nukta ya mwanzo katika mwale vilevile huitwa nukta ya mwisho, hivyo basi nukta A ni nukta ya mwisho ya mwale AC.

## Mfano wa 2

Miale ipi ni kinyume cha mingine katika mchoro ufuatao?





**Jibu**

Mwale AB na mwale AE ipo kinyume cha mwingine katika mchoro. Miale yote miwili inaanzia katika nukta A na kuendelea upande kinyume unaofanya mstari mnyoofu EB.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 3

Andika majina ya miale yote katika mchoro ufuatao.




**Jibu**

Katika mchoro huu kuna miale ifuatayo:
$\overrightarrow{AB}$, $\overrightarrow{AC}$, $\overrightarrow{BC}$, $\overrightarrow{AD}$, $\overrightarrow{AE}$, $\overrightarrow{DE}$, $\overrightarrow{AF}$, $\overrightarrow{AG}$ na $\overrightarrow{FG}$.

**Kazi ya kufanya 4:** Kuchora mstari mnyoofu


1. Tumia rula kuchora miale miwili; mmoja ukielekea kushoto na mwingine kuelekea kulia.
2. Unganisha nukta za mwanzo za miale miwili katika hatua ya 1 ili kupata mstari ulionyooka.

## Zoezi la 2

1. Chora vipande viwili vya mistari na utaje majina yake.
2. Chora mistari minyoofu mitatu, kisha taja majina yake.
3. Taja tofauti kati ya kipande cha mstari na mstari mnyoofu.
4. Je, unaweza kuchora kipande cha mstari cha sm 4 bila kutumia rula? Eleza sababu ya jibu lako.
5. Chora mwale XY na mwale YX.
6. Taja tofauti kati ya kipande cha mstari na mwale.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. Urefu wa kipande cha mstari chenye urefu wa sm 5 huweza kupimwa kwa kutumia kifaa gani?
8. Taja idadi ya vipande vya mistari katika mstari ufuatao:





9. Chora kipande cha mstari PQ, kisha taja idadi ya nukta za mwishoni.
10. Unganisha mwisho wa vipande vitatu vya mistari AB, BC na CA, kisha andika jina la umbo linalopatikana.
11. Je, unaweza kuchora miale mingapi kutoka kwenye nukta moja?
12. Taja mifano mitatu katika maisha ya kila siku ambayo inaweza kuwakilisha mwale.

## Kuunda maumbo bapa

Umbo bapa ni umbo lenye pande mbili za urefu na upana tu. Halina unene au kimo. Kuna aina nyingi za maumbo bapa ikiwemo mraba, mstatili, pembetatu, duara na mviringo.

**Kazi ya kufanya 5:** Kuunda maumbo bapa kwa kutumia nukta

1. Chunguza kwa makini nukta zifuatazo:




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Tumia penseli na rula kuunganisha nukta A na nukta B, C na D, A na D, na B na C.
3. Pima na kurekodi urefu wa vipande vya mistari $\overline{AB}$, $\overline{AD}$, $\overline{CD}$ na $\overline{BC}$.
4. Andika jina la umbo linalopatikana katika hatua ya 2.

## Zoezi la 3

1. Kuna vipande vya mstari vingapi katika umbo la pembetatu?
2. Unganisha nukta E, F, G na H ili kutengeneza maumbo bapa yafuatayo:
   (a) Pembetatu mbili.
   (b) Pembetatu nne.




3. Tiara inaundwa kwa vipande vingapi vya mstari?
4. Mchoro ufuatao una vipande vya mstari vingapi?





FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Majina ya maumbo bapa

Maumbo bapa hupewa majina kutokana na muundo, pembe au pande zake. Michoro ifuatayo inaonesha baadhi ya maumbo bapa na majina yake:




Pembetatu




Mraba




Mstatili



Duara



Pentagoni



Heksagoni

Mraba na mstatili ni maumbo bapa ambayo kila moja lina pande nne. Utofauti wa maumbo haya ni kuwa pande zote za mraba zina urefu unaolingana. Katika mstatili, pande zinazotazamana zina urefu unaolingana.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya 6:** Kuchora maumbo bapa kwa kutumia TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano)

1. Bainisha programu yoyote ya kompyuta inayotumika kuchora maumbo bapa.
2. Tumia programu uliyoibainisha katika hatua ya 1 kuchora maumbo ya mraba, pembetatu, duara na mstatili.
3. Chora maumbo bapa matano tofauti yenye pande tano.
4. Chora maumbo mengi zaidi kuimarisha umahiri wako.

**Mfano**

Chunguza michoro ifuatayo, kisha taja jina la umbo bapa linalohusika:

(a)




(b)



(c)



(d)





**Majibu**

(a) Umbo lina pande nane linaitwa oktagoni.
(b) Umbo lina pande nne linaitwa mstatili.
(c) Umbo lina pande tatu linaitwa pembetatu.
(d) Umbo linaitwa duara.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Zoezi la 4

1. Chunguza maumbo bapa a hadi j, kisha jibu maswali yanayofuata.




(a) Chora maumbo yote yenye pembe nne.
(b) Maumbo mangapi ni pembetatu?
(c) Taja maumbo ambayo ni duara.
(d) Tengeneza maumbo yaliyoainishwa kwa herufi a, b, d, e na f kwa kukata karatasi au manila.

2. Mchoro ufuatao ni kielelezo cha nyumba iliyotengenezwa kwa maumbo bapa. Chora maumbo bapa yote yaliyopo kwenye mchoro.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya 7

Kujifunza zaidi kutambua maumbo kwa kutumia masomo ya mtandaoni

### Maelezo

Tumia masomo ya mtandaoni kama vile video na michezo kutambua aina mbalimbali za maumbo bapa na kuyafananisha na vitu halisi vinavyopatikana katika mazingira yako.

### Jikumbushe

1. Maumbo bapa ni pamoja na mraba, mstatili, pembetatu na heksagoni
2. Pande zote za mraba zina urefu ulio sawa. Pande zinazotazamana katika mstatili zina urefu ulio sawa
3. Kipande cha mstari huchorwa kwa kuunganisha nukta mbili tofauti
4. Mwale una nukta ya kuanzia na unaendelea bila kikomo kwa kuwekwa mshale kuonesha uelekeo

### Msamiati


| | |
|---|---|
| Heksagoni | Umbo lenye pembe sita na pande sita zinazofanana. |
| Mraba | Umbo la pembe nne ambalo pande zake zote zinalingana. |
| Mstatili | Umbo lenye pembe nne ambalo pande mbili zinazotazamana zina urefu unaolingana. |

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la marudio


1. Chora vipande viwili vya mistari vyenye urefu wa sm 4 na sm 5.
2. Chora mwale PQ.
3. Mwale una nukta ngapi za kikomo?
4. Andika majina ya miale inayopatikana katika mchoro ufuatao.




5. Umbo lifuatalo lina mistari minyoofu mingapi?



6. Andika majina ya mistari minyoofu katika mchoro ufuatao.




7. Maumbo yafuatayo yana pembe ngapi?
   (a) Pembetatu (b) Pentagoni
   (c) Heksagoni


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Chora maumbo bapa mawili.

9. Katika michoro ifuatayo, maumbo gani siyo mstatili? Andika sababu ya jibu lako.


(a)



(b)




(c)



(d)




10. Kuna pembetatu ngapi katika umbo lifuatalo?



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


11. Chunguza mchoro ufuatao, kisha jibu maswali yanayofuata.



(a) Kuna vipande vya mistari vingapi katika mchoro?

(b) Taja majina ya maumbo bapa yanayopatikana katika mchoro.

12. Chunguza mchoro ufuatao, kisha jibu maswali yanayofuata:




(a) Taja majina ya nukta.

(b) Taja majina ya vipande vya mistari.

(c) Taja majina ya miale.

(d) Taja majina ya mistari minyoofu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sura ya Tano

# Sehemu

**Utangulizi**

*Katika sura hii utatumia mgawanyo wa vitu au makundi kujifunza sehemu. Aidha, utajumlisha na kutoa sehemu zenye asili moja. Umahiri utakaoujenga utakusaidia kugawa vitu mbalimbali kama vile dawa, vyakula na fedha, pamoja na kupata jumla au tofauti za sehemu.*

## Kutambua sehemu

Sehemu ni vipande vinavyounda kitu kizima. Kwa mfano, unapokata chungwa katika vipande na kuwagawia rafiki zako. Kila kipande huitwa sehemu. Sehemu huandikwa kama hivi, $\frac{1}{2}$, $\frac{1}{3}$ au $\frac{2}{5}$. Namba ya juu huitwa kiasi na namba ya chini huitwa asili.

### Kazi ya kufanya 1: Utambuzi wa sehemu


**Hatua**


1. Andaa kisu, kalamu za rashasha na chungwa au tikitimaji.
2. Tumia kisu kukata chungwa au tikitimaji katika vipande vilivyo sawa. Anza kwa kukata chungwa au tikitimaji katika vipande viwili, kisha kata vipande vinne vilivyo sawa.
3. Hesabu idadi ya vipande ulivyopata katika hatua ya 2.
4. Tumia kalamu ya rashasha kuweka alama katika kila kipande kulingana na sehemu yake.
5. Rudia hatua ya 2, 3 na 4 kukata machungwa au tikitimaji katika sehemu tofauti. Mfano robo, theluthi au moja ya tano.


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Mfano wa 1


Andika kwa numerali sehemu ya kila umbo iliyotiwa kivuli.


(a) 

(b) 

(c) 

(d) 

(e) 

(f) 

**Jibu**

(a) $\frac{1}{2}$ (b) $\frac{1}{3}$ (c) $\frac{2}{3}$ (d) $\frac{1}{8}$ (e) $\frac{4}{4}$ (f) $\frac{3}{8}$

## Mfano wa 2

Mama aliwapa watoto wake watatu maembe kama ifuatavyo: Rashidi alipata maembe 2, Upendo 2 na Likweme 2. Je, maembe aliyopata Rashidi ni sehemu gani ya maembe yote?

**Njia**

Rashidi maembe 2

Upendo maembe 2

Likweme maembe 2

Jumla ya maembe: $2 + 2 + 2 = 6$

Kwa hiyo, Rashidi alipata $\frac{2}{6}$ ya maembe yote.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

1. Chora duara, kisha ligawanye na utie kivuli kuonesha sehemu zifuatazo:
   (a) $\frac{1}{8}$ (b) $\frac{2}{3}$ (c) $\frac{3}{4}$

2. Kuna $\frac{1}{3}$ ngapi katika kitu kizima?

3. Kuna $\frac{1}{5}$ ngapi katika kitu kizima?




4. Musa alikata chungwa katika vipande viwili vilivyo sawa kama ilivyooneshwa kwenye mchoro ufuatao. Alimpa dada yake Neema kipande kimoja. Je, kila mmoja alipata sehemu gani ya chungwa?




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Tia kivuli katika mchoro (a) hadi (e) kuonesha sehemu husika

| | | |
|---|---|---|
| (a) |  | $\frac{2}{4}$ |
| (b) |  | $\frac{1}{3}$ |
| (c) |  | $\frac{6}{8}$ |
| (d) |  | $\frac{3}{5}$ |
| (e) |  | $\frac{5}{12}$ |

6. Andika jina la sehemu iliyotiwa kivuli katika michoro (a) hadi (d):

(a) 


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


(b)



(c)



(d)



7. Musa aligawanya mche wa sabuni katika sehemu nne zilizo sawa. Alimpa dada yake kipande kimoja. Je, alimpa sehemu gani ya mche huo?
8. Mbuzi wawili ni sehemu gani ya mbuzi sita?
9. Kuna maembe manane, kati ya hayo mawili ni mabovu. Maembe mabovu ni sehemu gani ya maembe yote?
10. Mkulima amechuma mapapai sita anataka kuwagawia watoto wake watatu kwa usawa. Je, kila mtoto atapata sehemu gani ya mapapai yote?
11. Selemani alikuwa na papai moja. Aliamua agawane papai hilo na rafiki zake wawili katika vipande vilivyo sawa. Je, kila moja alipata sehemu gani ya papai hilo?
12. Sadiki ana ndizi ishirini. Anataka kuwapa ndizi watoto wake wanne kwa usawa. Je, kila mtoto atapata sehemu gani ya ndizi zote?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kujumlisha sehemu zenye asili moja


*Ili kuongeza sehemu zenye asili moja, ongeza kiasi tu na asili isibadilike.*

### Mfano wa 1

*Tumia michoro kujibu swali lifuatalo:* $\frac{3}{4}+\frac{1}{4}=$

**Hatua**

1. *Chora robo tatu ya duara na tia kivuli.*
2. *Andika sehemu iliyotiwa kivuli kwa numerali*
3. *Chora robo duara na tia kivuli.*
4. *Andika kwa numerali sehemu iliyotiwa kivuli*
5. *Jumlisha idadi ya sehemu zilizotiwa kivuli kupata umbo la duara.*
6. *Chora na tia kivuli kuonesha jumla ya robo tatu na robo.*
7. *Andika sehemu iliyotiwa kivuli kwa numerali.*




*Jibu ni duara moja lililotiwa kivuli na kugawanywa katika sehemu nne zilizo sawa. Kujumlisha sehemu zenye asili moja, jumlisha kiasi kama unavyojumlisha namba za kawaida. Asili haibadiliki kwa kuwa sehemu zinaunda kitu kimoja.*

*Hivyo,* $\frac{3}{4}+\frac{1}{4}=\frac{3+1}{4}=\frac{4}{4}$.

*Kwa hiyo,* $\frac{3}{4}+\frac{1}{4}=\frac{4}{4}$.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 2

$\frac{13}{27}+\frac{7}{27}=$

**Njia**

*Jumlisha namba za kiasi kama unavyojumlisha namba za kawaida, asili haibadiliki.*

Hivyo, $\frac{13}{27}+\frac{7}{27}=\frac{13+7}{27}=\frac{20}{27}$.

Kwa hiyo, $\frac{13}{27}+\frac{7}{27}=\frac{20}{27}$.

## Zoezi la 2

1. *Jibu maswali yafuatayo bila kutumia michoro:*

(a) $\frac{2}{5}+\frac{2}{5}=$

(b) $\frac{3}{9}+\frac{5}{9}=$

(c) $\frac{1}{4}+\frac{1}{4}=$

(d) $\frac{3}{6}+\frac{2}{6}=$

(e) $\frac{1}{5}+\frac{2}{5}=$

(f) $\frac{5}{8}+\frac{1}{8}=$

(g) $\frac{3}{10}+\frac{5}{10}=$

(h) $\frac{1}{7}+\frac{5}{7}=$

(i) $\frac{1}{2}+\frac{1}{2}=$

(j) $\frac{2}{6}+\frac{4}{6}=$

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(k) $\frac{1}{4}+\frac{2}{4}=$

(l) $\frac{1}{15}+\frac{6}{15}=$

(m) $\frac{3}{9}+\frac{4}{9}=$

(n) $\frac{3}{7}+\frac{3}{7}=$

(o) $\frac{0}{5}+\frac{2}{5}=$

(p) $\frac{1}{3}+\frac{1}{3}=$

(q) $\frac{2}{7}+\frac{4}{7}=$

(r) $\frac{11}{20}+\frac{7}{20}=$

(s) $\frac{1}{10}+\frac{3}{10}=$

(t) $\frac{16}{35}+\frac{9}{35}=$

2. Jibu maswali yafuatayo kwa kutumia michoro:

(a) $\frac{2}{4}+\frac{0}{4}=$

(b) $\frac{1}{3}+\frac{1}{3}=$

(c) $\frac{3}{8}+\frac{1}{8}=$

(d) $\frac{2}{5}+\frac{1}{5}=$

(e) $\frac{4}{6}+\frac{2}{6}=$

(f) $\frac{5}{7}+\frac{1}{7}=$

(g) $\frac{2}{10}+\frac{5}{10}=$

(h) $\frac{4}{9}+\frac{3}{9}=$

(i) $\frac{5}{15}+\frac{7}{15}=$

(j) $\frac{6}{20}+\frac{3}{20}=$

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mafumbo yenye dhana ya kujumlisha sehemu

### Mfano wa 1

Yona alijaza maji $\frac{3}{9}$ ya pipa na Halima alijaza $\frac{2}{9}$ ya pipa hilo. Je, Yona na Halima kwa pamoja walijaza sehemu gani ya pipa hilo?

**Njia**

Yona alijaza maji $\frac{3}{9}$ ya pipa

Halima alijaza maji $\frac{2}{9}$ ya pipa

Wote walijaza: $\frac{3}{9}+\frac{2}{9}=\frac{3+2}{9}=\frac{5}{9}$.

Kwa hiyo, Yona na Halima walijaza maji $\frac{5}{9}$ ya pipa hilo.

### Mfano wa 2

Nyumbani kulikuwa na mfuko mmoja wa sukari. Anna alitumia $\frac{3}{8}$ ya sukari na Yahaya alitumia $\frac{4}{8}$ ya sukari katika mfuko huo. Je, jumla walitumia sehemu gani ya sukari?

**Njia**

Anna alitumia $\frac{3}{8}$ ya sukari na Yahaya alitumia $\frac{4}{8}$ ya sukari

Jumla walitumia: $\frac{3}{8}+\frac{4}{8}=\frac{3+4}{8}=\frac{7}{8}$.

Kwa hiyo, walitumia $\frac{7}{8}$ ya sukari katika mfuko huo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

1. Mama alimpa mwanae robo ya chapati. Baadaye alimpa robo tatu ya chapati hiyo. Jumla alimpatia sehemu gani ya chapati hiyo?

2. Masanja alikula $\frac{1}{6}$ ya mkate na Amani alikula $\frac{2}{6}$ ya mkate huo. Ni sehemu gani ya mkate huo walikula wote wawili?

3. Mkulima aligawa shamba lake katika sehemu nane. Alitumia $\frac{4}{8}$ ya shamba hilo kupanda mbegu za mahindi, na $\frac{3}{8}$ kupanda mbegu za maharage. Je, ni sehemu gani ya shamba hilo alipanda mbegu za mahindi na maharage?

4. Wanakijiji waliuza $\frac{2}{5}$ ya pamba yao kwenye chama chao cha ushirika. Pia, $\frac{3}{5}$ ya pamba yao iliuzwa kwenye chama kingine cha ushirika. Je, wanakijiji waliuza sehemu gani ya pamba yote?

5. Tausi alitumia $\frac{1}{7}$ ya mshahara wake kulipia kodi. Pia, alitumia $\frac{3}{7}$ ya mshahara kwa chakula. Je, alitumia sehemu gani ya mshahara wake wote?

6. Maunda alinunua samaki wawili. Mmoja alikuwa na uzani wa $\frac{2}{4}$ ya kilogramu na mwingine $\frac{2}{4}$ ya kilogramu. Tafuta jumla ya uzani wa samaki hao.

7. Wakazi wa kijiji cha Maendeleo walitaka kujenga kituo cha afya. Wanakijiji hao walifyatua $\frac{5}{10}$ ya matofali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

yaliyohitajika na $\frac{3}{10}$ ya matofali yalitolewa na mwenyekiti wa kijiji. Je, kijiji hicho kina sehemu gani ya matofali yote yanayohitajika?

8. Nuru aliuza $\frac{3}{10}$ ya machungwa siku ya kwanza na $\frac{6}{10}$ ya machungwa siku ya pili. Kwa siku mbili aliuza sehemu gani ya machungwa?

9. Shule ilinunua vitabu. Kati ya vitabu hivyo $\frac{4}{12}$ vilikuwa vya Hisabati, $\frac{2}{12}$ vya Kiswahili na $\frac{3}{12}$ vya Sayansi na Teknolojia. Vitabu hivyo vya masomo matatu ni sehemu gani ya vitabu vyote vilivyonunuliwa?

10. Mama Jeni alinunua keki kwa ajili ya siku yake ya kuzaliwa. Akaikata hiyo vipande sita vilivyo sawa na kumpa Jeni vipande viwili. Je, Jeni alipewa sehemu gani ya ile keki?

## Kutoa sehemu zenye asili moja

Ili kuweza kutoa sehemu zenye asili moja, toa kiasi tu na asili isibadilike.

### Mfano wa 1

Tumia michoro kutafuta jibu sahihi la swali lifuatalo:


$\frac{3}{3} - \frac{1}{3} =$

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Hatua**

1. Chora duara na gawanya duara hilo katika vipande vitatu vilivyo sawa.
2. Tia kivuli vipande vitatu kwenye duara hilo na andika sehemu iliyotiwa kivuli kwa numerali.
3. Ondoa kipande kimoja ulichotia kivuli katika hatua ya pili. Andika sehemu ya kipande hicho kwa numerali.
4. Chora tena kuonesha sehemu ya duara iliyobaki katika hatua ya tatu baada ya kuondoa kipande kimoja.
5. Andika sehemu iliyobaki katika hatua ya nne kwa numerali.

Hatua za awali zinaweza kuoneshwa kama ifuatavyo:



$\frac{3}{3} - \frac{1}{3} = \frac{2}{3}$

Kutoa sehemu zenye asili moja. Toa kiasi kama unavyotoa namba za kawaida.

Asili haibadiliki kwa kuwa sehemu zinaunda kitu kimoja.

Hivyo: $\frac{3}{3} - \frac{1}{3} = \frac{3-1}{3} = \frac{2}{3}$.

Kwa hiyo, $\frac{3}{3} - \frac{1}{3} = \frac{2}{3}$.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Mfano wa 2

Kwa kutumia mchoro tafuta jibu sahihi la swali lifuatalo.

$\frac{5}{6} - \frac{1}{6} =$

**Hatua**

1. Chora tano ya sita ya duara.
2. Andika sehemu ya duara iliyotiwa kivuli kwa numerali.
3. Ondoa kipande kimoja ulichotia kivuli kwenye duara.
4. Andika kwa numerali sehemu uliyoiondoa.
5. Chora nne ya sita sehemu ya duara iliyobaki.
6. Andika kwa numerali sehemu ya duara iliyobaki.




$\frac{5}{6}$ – $\frac{1}{6}$ = $\frac{4}{6}$

Hivyo, $\frac{5}{6} - \frac{1}{6} = \frac{5-1}{6} = \frac{4}{6}$.

Kwa hiyo, $\frac{5}{6} - \frac{1}{6} = \frac{4}{6}$.

## Mfano wa 3

Tafuta thamani ya $\frac{11}{12} - \frac{7}{12} =$

**Njia**

Toa kiasi kama unavyotoa namba, ukizingatia kuwa asili huwa haibadiliki.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hivyo, $\frac{11}{12}-\frac{7}{12}=\frac{11-7}{12}=\frac{4}{12}$.

Kwa hiyo, $\frac{11}{12}-\frac{7}{12}=\frac{4}{12}$.

## Zoezi la 4

1. $\frac{5}{8}-\frac{3}{8}=$
2. $\frac{2}{5}-\frac{1}{5}=$
3. $\frac{4}{9}-\frac{1}{9}=$
4. $\frac{6}{7}-\frac{4}{7}=$
5. $\frac{2}{3}-\frac{1}{3}=$
6. $\frac{14}{14}-\frac{1}{14}=$
7. $\frac{3}{6}-\frac{1}{6}=$
8. $\frac{7}{8}\ \frac{5}{8}=$
9. $\frac{6}{13}-\frac{3}{13}=$
10. $\frac{3}{5}-\frac{2}{5}=$
11. $\frac{4}{5}-\frac{1}{5}=$
12. $\frac{5}{7}-\frac{3}{7}=$
13. $\frac{2}{6}-\frac{2}{6}=$
14. $\frac{2}{2}-\frac{1}{2}=$
15. $\frac{5}{10}-\frac{2}{10}=$
16. $\frac{4}{4}-\frac{2}{4}=$
17. $\frac{5}{11}-\frac{1}{11}=$
18. $\frac{16}{50}-\frac{5}{50}=$
19. $\frac{24}{25}-\frac{20}{25}=$
20. $\frac{75}{100}-\frac{50}{100}=$
21. $\frac{35}{40}-\frac{25}{40}=$
22. $\frac{41}{75}-\frac{23}{75}=$
23. $\frac{17}{20}-\frac{9}{20}=$
24. $\frac{75}{100}-\frac{25}{100}=$
25. $\frac{24}{40}-\frac{20}{40}=$

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mafumbo yenye dhana ya kutoa sehemu

### Mfano wa 1

Tano ya nane ya shamba imepandwa miti ya mikaratusi. Sehemu ya shamba iliyobaki imepandwa miti ya michungwa. Sehemu gani ya shamba imepandwa miti ya michungwa?

**Njia**

Shamba lote limegawanywa katika vipande 8; Sawa na $\frac{8}{8}$.

Sehemu iliyopandwa miti ya mikaratusi ni $\frac{5}{8}$.

Sehemu iliyopandwa miti ya michungwa = shamba lote – sehemu iliyopandwa miti ya mikaratusi.

$$\frac{8}{8} - \frac{5}{8} = \frac{8}{8} - \frac{5}{8} = \frac{8-5}{8} = \frac{3}{8}.$$

Kwa hiyo, sehemu ya shamba iliyopandwa miti ya michungwa ni $\frac{3}{8}$.

### Mfano wa 2

Katu alifanya nne ya kumi na mbili ya usafi wa darasa lake. Je, ni sehemu gani ya darasa haikufanyiwa usafi?

**Njia**

Darasa lote lina sehemu 12; sawa na $\frac{12}{12}$.

Sehemu iliyofanyiwa usafi ni $\frac{4}{12}$.

Sehemu ambayo haikufanyiwa usafi = darasa lote – sehemu iliyofanyiwa usafi.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

$\frac{12}{12} - \frac{4}{12} = \frac{12}{12} - \frac{4}{12} = \frac{12-4}{12} = \frac{8}{12}$.

Kwa hiyo, sehemu ya darasa ambayo haikufanyiwa usafi ni $\frac{8}{12}$.

## Zoezi la 5

1. Nusu ya shamba la Ngosha limelimwa. Je, ni sehemu gani ya shamba halijalimwa?
2. Aisha alivuna machungwa kutoka katika shamba lake. Ikiwa robo ya machungwa hayo yaliharibika, ni sehemu gani ya machungwa hayakuharibika?
3. Bahati alikata tikitimaji katika vipande 10 vinavyolingana. Iwapo vipande 7 kati ya 10 viliuzwa, ni sehemu gani ya tikitimaji haikuuzwa?
4. Mariam alikula moja ya sita ya muwa wote. Je, ni sehemu gani ya muwa ilibakia?
5. Kandi alikuwa na $\frac{5}{9}$ ya mkate. Akampatia Ali $\frac{4}{9}$ ya mkate huo. Je, alibakiwa na sehemu gani ya mkate?
6. Kabula alijibu $\frac{7}{12}$ ya maswali ya Hisabati asubuhi na $\frac{2}{12}$ ya maswali hayo mchana. Je, ni sehemu gani ya maswali ilibakia?
7. Johari alivuna $\frac{3}{10}$ ya vitunguu katika shamba. Debora alivuna $\frac{4}{10}$ ya vitunguu katika shamba hilo hilo. Nini tofauti ya sehemu ya vitunguu walivyovuna?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Robo tatu ya shamba la Kwame ni sehemu inayopakana na barabara kuu. Sehemu gani ya shamba la Kwame haipakani na barabara kuu?

9. Bakari alitumia $\frac{1}{10}$ ya mshahara wake kulipa kodi ya nyumba na $\frac{2}{10}$ kwa kulipa bili ya maji na umeme. Bakari alibakiwa na sehemu gani ya mshahara wake?

10. Wanakijiji walipanda miche ya miti ya matunda. Iwapo $\frac{2}{7}$ ya miti yote ilikauka, sehemu gani ya miti ilistawi?

## Kazi ya kufanya 2

Kujifunza zaidi sehemu kwa njia ya masomo ya mtandaoni

### Maelezo

Tumia masomo ya mtandaoni:

1. Kuonesha sehemu. Mfano $\frac{1}{2}$, $\frac{1}{3}$, $\frac{2}{3}$, $\frac{1}{4}$, $\frac{3}{4}$.

2. Kuchora maumbo mbalimbali, kuyagawanya katika sehemu zilizo sawa, kisha kutia kivuli na kuonesha sehemu iliyotiwa kivuli kwa namba.

### Jikumbushe

1. Baadhi ya sehemu za maumbo zina majina maalumu, mfano $\frac{1}{4}$ inaitwa ni robo, $\frac{1}{2}$ ni nusu na $\frac{1}{3}$ ni theluthi

2. Namba iliyo juu ya mstari wa kugawanya huitwa kiasi na iliyo chini ya mstari huitwa asili

3. Kujumlisha na kutoa sehemu zenye asili moja, asili huwa haibadiliki

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Msamiati | | |
|---|---|---|
| Nusu | $= \frac{1}{2}$ | Kipande kimoja kati ya vipande viwili vilivyo sawa vya kitu kizima |
| Robo | $= \frac{1}{4}$ | Kipande kimoja kati ya vipande vinne vilivyo sawa vya kitu kizima |
| Robo tatu | $= \frac{3}{4}$ | vipande vitatu kati ya vipande vinne vilivyo sawa vya kitu kizima |
| Theluthi | $= \frac{1}{3}$ | Kipande kimoja kati ya vipande vitatu vilivyo sawa vya kitu kizima |
| Theluthi mbili | $= \frac{2}{3}$ | vipande viwili kati ya vipande vitatu vilivyo sawa vya kitu kizima |

## Zoezi la Marudio

1. $\frac{3}{9} + \frac{5}{9} =$
2. $\frac{2}{5} + \frac{2}{5} =$
3. $\frac{2}{6} + \frac{3}{6} =$
4. $\frac{3}{20} + \frac{3}{20} =$
5. $\frac{3}{6} - \frac{1}{6} =$
6. $\frac{3}{10} + \frac{5}{10} =$
7. $\frac{9}{16} + \frac{2}{16} =$
8. $\frac{3}{5} + \frac{2}{5} =$
9. $\frac{2}{6} - \frac{2}{6} =$
10. $\frac{4}{10} + \frac{5}{10} =$
11. $\frac{25}{25} - \frac{20}{25} =$
12. $\frac{35}{50} - \frac{10}{50} =$

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

13. $\frac{5}{8} - \frac{1}{8} =$

14. $\frac{6}{7} - \frac{4}{7} =$

15. $\frac{3}{25} + \frac{4}{25} =$

16. $\frac{6}{20} + \frac{11}{20} =$

17. $\frac{9}{15} + \frac{2}{15} =$

18. $\frac{8}{9} + \frac{1}{9} =$

19. $\frac{6}{7} - \frac{2}{7} =$

20. $\frac{30}{30} - \frac{15}{30} =$


21. $\frac{13}{50} + \frac{30}{50} =$

22. $\frac{40}{100} - \frac{16}{100} =$


23. $\frac{15}{35} - \frac{6}{35} =$

24. Andika kwa numerali sehemu iliyotiwa kivuli katika mchoro (a) hadi (c):


(a)



(b)



(c)



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

25. Jakobo alinunua kuku wawili. Mmoja alikuwa na uzani wa $\frac{2}{4}$ ya kilogramu na mwingine $\frac{2}{4}$ ya kilogramu. Tafuta jumla ya uzani wa kuku hao.

26. Moja ya sita ya pipa lilijazwa maji. Je, ni sehemu gani ya pipa haikujazwa maji?

27. John alikata nanasi katika vipande 20 vinavyolingana. Iwapo $\frac{17}{20}$ ya nanasi hilo iliuzwa, ni sehemu gani ya nanasi haikuuzwa?

28. Wanafunzi wa darasa la tatu katika shule fulani wana mabegi ya bluu na meusi. Ikiwa $\frac{1}{3}$ ya wanafunzi wana mabegi ya bluu, je ni sehemu gani ya wanafunzi wa darasa hilo wana mabegi meusi?

29. Mwalimu anataka kuwagawia wanafunzi wanne muwa wenye pingili nne zilizo sawa. Je, kila mwanafunzi atapata sehemu gani ya muwa huo?



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

30. Wanafunzi wa darasa la 3A walipewa zoezi la Hisabati. Ikiwa $\frac{35}{40}$ ya wanafunzi hao walifanya zoezi hilo. Je, ni sehemu gani ya wanafunzi hawakufanya zoezi?

31. Wanafunzi walilima $\frac{4}{10}$ ya bustani siku ya kwanza na $\frac{5}{10}$ ya bustani siku ya pili. Je, wanafunzi hao walilima sehemu gani ya bustani kwa siku mbili hizo?

32. Burhani alikuwa na tufaa 8. Ikiwa $\frac{5}{8}$ ya tufaa zake ziliharibika, je, alibakiwa na sehemu gani ya tufaa zilizokuwa nzima?

33. Ali alitumia $\frac{4}{7}$ ya fedha zake kununua nguo na $\frac{1}{7}$ kununua vitabu. Je, alibakiwa na sehemu gani ya fedha zake?

34. Fatuma alimpa Rozi $\frac{2}{5}$ ya pipi zake. Pia, alimpa Kabela $\frac{1}{5}$ ya pipi zake. Je, Fatuma aliwapa Rozi na Kabela sehemu gani ya pipi zake?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sura ya Sita

# Vipimo vya muda


**Utangulizi**

*Katika sura hii, utajifunza vipimo vya muda. Utasoma muda kwa mtindo wa saa 12 na saa 24. Pia, utajifunza kutambua idadi ya saa katika siku, siku katika wiki, wiki katika mwezi na miezi katika mwaka. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kupanga na kuzingatia muda katika shughuli mbalimbali. Shughuli hizo ni pamoja na kufuatilia ratiba ya shule, vyombo vya habari na vyombo vya usafiri.*

## Vipimo vya muda

Muda hupimwa kwa sekunde, dakika, saa, siku, wiki, mwezi au mwaka. Uhusiano wa vipimo vya muda ni kama ifuatavyo:

(a) Dakika moja ina sekunde 60.
(b) Saa moja ina dakika 60.
(c) Siku moja ina saa 24.
(d) Wiki moja ina siku 7.
(e) Mwaka mmoja una miezi 12.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vipimio vya muda

Vipimio vya muda vinaweza kuwa saa au kalenda. Kuna aina mbili za saa ambazo ni saa ya mshale na saa ya kidigiti. Saa hutumika kupima muda kwa saa ishirini na nne za siku, Kalenda hutumika kupima siku, wiki na miezi katika mwaka.



Saa ya mshale




Saa ya kidigiti




Kalenda

### Zoezi la 1

Jedwali lifuatalo linaonesha matokeo ya muda waliotumia wanafunzi wanne kusimama kwa mguu mmoja katika mchezo wao. Soma muda huo, kisha jibu maswali yanayofuata.


| Jina | Muda |
|---|---|
| Musa | Dakika 1 na sekunde 24 |
| Neema | Dakika 1 na sekunde 40 |
| Sofia | Sekunde 103 |
| Hassan | Dakika 1 na sekunde 36 |

1. Nani alitumia muda mrefu kuliko wote?
2. Nani alitumia muda mfupi kuliko wote?
3. Neema alitumia sekunde ngapi?
4. Musa alitumia sekunde ngapi?
5. Hassan alitumia sekunde ngapi?
6. Sofia alitumia dakika na sekunde ngapi?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kusoma muda kwa mtindo wa saa 12

Katika kusoma saa ya mshale, mshale mfupi ni mshale wa saa. Mshale unaofuata kwa urefu ni mshale wa dakika. Mshale ulio mrefu zaidi na mwembamba ni mshale wa sekunde. Mishale yote huzunguka uso wa saa kuanzia kushoto kuelekea kulia.





Katika saa ya kidigiti, saa na dakika hutenganiswa na nukta pacha (:). Tarakimu mbili za mwanzo kushoto huonesha saa. Tarakimu mbili zanazofuata huonesha dakika kama inavyooneshwa katika mchoro ufuatao:




FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Chunguza mchoro ufuatao:





Dakika 60 ni saa moja

Mshale wa dakika hutumia dakika tano kuzunguka kutoka namba moja hadi nyingine kwenye uso wa saa. Muda wa dakika 30 husomwa kama nusu saa, dakika 15 husomwa kama robo saa. Hii imeoneshwa katika michoro ifuatayo.




Dakika 30 ni nusu saa




Dakika 15 ni robo saa


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 1

Chora uso wa saa ya mshale unaoonesha saa 4:00.

**Hatua**

1. Andaa kitu cha duara kama sarafu ya shilingi 200 au 500.
2. Weka kitu hicho cha duara kwenye karatasi na tumia penseli kuchora duara kwa kuzungushia.
3. Weka alama 12 kwa kuacha nafasi zinazolingana kama zinavyoonekana katika duara lifuatalo.




4. Andika namba 1, 2, 3 hadi 12 kwenye alama ulizoweka.
5. Chora mshale mfupi kuanzia katikati kulenga namba 4.
6. Chora mshale mrefu kuanzia katikati kulenga namba 12.
7. Chora mshale mrefu wa sekunde katikati kulenga namba 12.




8. Uso wa saa unaonesha saa 4.00.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kusoma muda katika saa na dakika

*Kusoma dakika anzia kwenye 12, kisha soma dakika kuelekea kulia hadi mshale wa dakika unapoonesha. Anza kusoma saa, kisha dakika.*

### Mfano wa 2

*Chora uso wa saa ya mshale kuonesha saa saba na dakika kumi na tano au saa saba na robo au saa 7:15.*




### Mfano wa 3

*Chunguza nyuso za saa za mshale na saa za kidigiti, kisha soma muda unaooneshwa.*

(a)




(b)




(c)




**Jibu**

(a) Saa 1 kamili (b) Saa 2 kamili (c) Saa 6 kamili

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 4

Soma saa za mshale zisizo na namba na za kidigiti, kisha andika muda wa saa hizo.

(a)




(b)




(c)




**Jibu**

(a) Saa moja na dakika kumi na tano

(b) Saa kumi na dakika thelathini

(c) Saa nane na dakika arobaini na tano


## Mfano wa 5

Soma muda katika saa zifuatazo, kisha andika muda wa saa hizo kwa numerali na kwa maneno:

(a)




(b)



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c)



(d)




(e)




(f)



(g)




(h)



(i)



(j)



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Majibu**

(a) Saa 10 na dakika 10 (10:10).

(b) Saa 6 na dakika 20 (6:20).

(c) Saa 7 na dakika 35 (7:35).au saa 8 kasoro dakika 25.

(d) Saa 2 na dakika 5 (2:05).

(e) Saa 12 na dakika 45 au saa 1 kasoro robo (saa 1 kasoro dakika 15 au 12:45)

(f) Saa 5 na dakika 45 au saa 6 kasoro robo (saa 6 kasoro dakika au 5:45)

(g) Saa 9 na dakika 45 (9:45) au saa 10 kasoro robo (saa 10 kasoro dakika 15)

(h) Saa 2 na dakika 50 (2:50) au saa 3 kasoro dakika 10

(i) Saa 6 na dakika 40 (6:40) au saa 7 kasoro dakika 20

(j) Saa 4 na dakika 55 (4:55) au saa 5 kasoro dakika 05

## Zoezi la 2

1. Chunguza nyuso za saa zifuatazo, kisha jibu maswali yafuatayo:

A




B




(a) Uso wa saa A ni wa aina gani?

(b) Uso wa saa B unaonesha muda gani?

(c) Uso wa saa A unaonesha muda gani?

(d) Kuna tofauti gani kati ya uso wa saa A na B?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Soma saa zifuatazo, kisha andika muda kwa numerali na kwa maneno.

(a)



(b)



(c)



(d)



(e)



(f)



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Chora mishale katika nyuso za saa kuonesha muda uliotajwa.

(a)



Saa 7 na dakika 5
(7:05)

(b)



Saa 2 na dakika 35
(2:35)

(c)



Saa 6 na dakika 55 au
saa 7 kasoro dakika 5
(6:55)

(d)



Saa 2 na dakika 45 au
Saa 3 kasoro robo (2:45)

4. Andika muda kwa maneno.

(a) 8:45 _____

(b) 12:10 _____

(c) 11:40 _____

(d) 2:25 _____

(e) 4:35 _____

(f) 5:05 _____

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Chora uso wa saa ya mshale na ya kidigiti inayoonesha muda katika saa zifuatazo:
   (a) Saa saba kamili
   (b) Saa tisa kamili
   (c) Saa mbili na dakika thelathini
   (d) Saa tatu na dakika arobaini na tano.

6. Andika muda kwa numerali.
   (a) Saa moja na nusu _____
   (b) Saa nne na dakika ishirini na tano _____
   (c) Saa kumi na moja kamili _____
   (d) Saa sita na dakika arobaini na tano _____

## Kusoma muda kwa mtindo wa saa 24

Kielelezo kifuatacho kinaonesha saa 24 ambazo hazisomwi kwenye nyuso za saa za mshale.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Inafahamika kuwa mchana mmoja una saa 12 na usiku mmoja una saa 12. Katika mtindo wa saa 24, siku huanza baada ya saa 6:00 usiku. Mtindo wa saa 24 huandikwa kwa tarakimu nne. Tarakimu mbili za mwanzo kushoto huonesha saa na zilizobaki huonesha dakika.

Jedwali lifuatalo linaonesha uhusiano wa muda katika mtindo wa saa 12 na saa 24.

| Mtindo wa saa 12 | Mtindo wa saa 24 |
|---|---|
| 6:00 Usiku | Saa 0000 |
| 6:01 Usiku | Saa 0001 |
| 7:00 Usiku | Saa 0100 |
| 8:00 Usiku | Saa 0200 |
| 9:00 Usiku | Saa 0300 |
| 10:00 Alfajiri | Saa 0400 |
| 11:00 Alfajiri | Saa 0500 |
| 12:00 Asubuhi | Saa 0600 |
| 1:00 Asubuhi | Saa 0700 |
| 2:00 Asubuhi | Saa 0800 |
| 3:00 Asubuhi | Saa 0900 |
| 4:00 Asubuhi | Saa 1000 |
| 5:00 Asubuhi | Saa 1100 |
| 6:00 Adhuhuri | Saa 1200 |
| 6:01 Mchana | Saa 1201 |
| 7:00 Mchana | Saa 1300 |
| 8:00 Mchana | Saa 1400 |
| 9:00 Alasiri | Saa 1500 |
| 10:00 Jioni | Saa 1600 |
| 11:00 Jioni | Saa 1700 |
| 12:00 Jioni | Saa 1800 |
| 1:00 Usiku | Saa 1900 |
| 2:00 Usiku | Saa 2000 |
| 3:00 Usiku | Saa 2100 |
| 4:00 Usiku | Saa 2200 |
| 5:00 Usiku | Saa 2300 |
| 6:00 Usiku | Saa 0000 |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Mfano wa 1

Andika saa 6:30 mchana katika mtindo wa saa 24.

**Jibu**

Saa 6:30 mchana ni sawa na saa 1230 katika mtindo wa saa 24.

### Mfano wa 2

Andika 0235 katika mtindo wa saa 12.

**Jibu**

Saa 0235 ni sawa na 8:35 usiku katika mtindo wa saa 12.

### Mfano wa 3

Andika saa 4:45 usiku katika mtindo wa saa 24.

**Jibu**

Saa 4:45 usiku ni sawa na 2245 katika mtindo wa saa 24.

### Zoezi la 3

1. Badili saa 3:47 asubuhi kwenda katika mtindo wa saa 24.
2. Andika saa 8:00 mchana katika mtindo wa saa 24.
3. Andika saa 7:00 mchana katika mtindo wa saa 24.
4. Badili saa 0400 kuwa katika mtindo wa saa 12.
5. Andika saa 1700 kuwa katika mtindo wa saa 12.
6. Andika saa 2200 kuwa katika mtindo wa saa 12.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Zoezi la 4

1. Andika saa zifuatazo katika mtindo wa saa 24.
   (a) Saa 3:00 asubuhi (b) Saa 7:00 mchana
   (c) Saa 12:01 jioni (d) Saa 9:45 alasiri
   (e) Saa 5:00 asubuhi (f) Saa 10:00 jioni
   (g) Saa 6:50 usiku (h) Saa 2:00 asubuhi
   (i) Saa 2:34 asubuhi (j) Saa 11:55 alfajiri
2. Andika saa zifuatazo katika mtindo wa saa 12.
   (a) Saa 0012 (b) Saa 1710
   (c) Saa 1650 (d) Saa 0712
   (e) Saa 2010 (f) Saa 2324
   (g) Saa 1015 (h) Saa 0815
   (i) Saa 1918 (j) Saa 0000
3. Kuna saa ngapi kuanzia saa 1800 mpaka saa 0000?
4. Saa 2300 ni saa ngapi katika mtindo wa saa 12?
5. Sheba alimwambia Bura kuwa saa yake ilionesha saa 2:15 asubuhi. Je, hiyo ni saa ngapi katika mtindo wa saa 24?
6. Daktari alifanya kazi kwa saa 11. Iwapo alianza kazi saa 1:30 asubuhi, alimaliza kazi saa ngapi katika mtindo wa saa 24?
7. Watalii waliwasili uwanja wa ndege wa Kilimanjaro saa 1625. Andika muda huo katika mtindo wa saa 12.
8. Askari wa usalama barabarani aliwasili kituo cha Polisi saa 11:45 alfajiri. Je, aliwasili saa ngapi katika mtindo wa saa 24?
9. Asha alianza kupata maumivu ya kichwa siku ya Ijumaa saa1808. Andika muda huo katika mtindo wa saa 12.
10. Safia na Ramadhani huamka saa 12:30 asubuhi ili kujiandaa kwenda shule. Andika muda huo katika mtindo wa saa 24.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Uhusiano katika muda

Mchoro huu unaonesha uhusiano wa siku katika wiki, wiki katika mwezi na miezi katika mwaka.




Kumbuka kuwa muda hupimwa kwa siku, wiki, mwezi au mwaka.

(a) Siku moja ina saa 24.
(b) Wiki moja ina siku 7.
(c) Mwezi mmoja una wiki 4.
(d) Mwezi mmoja una siku 28, 29, 30 au 31.
(e) Mwaka mmoja una miezi 12.

### Majina ya siku katika wiki

Wiki moja ina siku saba. Majina ya siku hizo ni kama yanavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

| Majina ya siku katika wiki | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumatatu | Jumanne | Jumatano | Alhamisi | Ijumaa | Jumamosi | Jumapili |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Majina ya miezi katika mwaka

Mwaka mmoja una miezi kumi na mbili. Kila mwezi una jina lake kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo.

| Januari | Februari | Machi | Aprili |
|---|---|---|---|
| Mwezi wa 1 | Mwezi wa 2 | Mwezi wa 3 | Mwezi wa 4 |
| Siku 31 | Siku 28 au 29 | Siku 31 | Siku 30 |

| Mei | Juni | Julai | Agosti |
|---|---|---|---|
| Mwezi wa 5 | Mwezi wa 6 | Mwezi wa 7 | Mwezi wa 8 |
| Siku 31 | Siku 30 | Siku 31 | Siku 31 |

| Septemba | Oktoba | Novemba | Desemba |
|---|---|---|---|
| Mwezi wa 9 | Mwezi wa 10 | Mwezi wa 11 | Mwezi wa 12 |
| Siku 30 | Siku 31 | Siku 30 | Siku 31 |

### Zoezi la 5

1. Saa 24 ni sawa na siku ngapi?
2. Siku 7 ni sawa na wiki ngapi?
3. Mwezi mmoja una wiki ngapi?
4. Mwezi mmoja una siku ngapi?
5. Miezi 12 ni sawa na miaka mingapi?
6. Bakari alinunua muda wa maongezi ambao ulidumu kwa muda wa saa 48. Je, muda huu ni sawa na siku ngapi?

## Kalenda

Kalenda huonesha siku, wiki, mwezi na mwaka. Kalenda huonesha tarehe za matukio muhimu ya kitaifa na kimataifa. Kalenda hutuwezesha kujua aina ya mwaka iwapo ni mfupi au mrefu. Katika mwaka mrefu mwezi Februari huwa na siku 29. Mwaka mfupi mwezi Februari una siku 28.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zifuatazo ni kalenda za mwaka 2019 na mwaka 2020.

# 2019 Tanzania

**JANUARI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | | |

**FEBRUARI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | | |

**MACHI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | | | | | | |

**APRILI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | 30 | | | | |

**MEI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | |

**JUNI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |
| 30 | | | | | | |

**JULAI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | 30 | 31 | | | |

**AGOSTI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 |
| 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 |

**SEPTEMBA**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 |
| 29 | 30 | | | | | |

**OKTOBA**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | | |

**NOVEMBA**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |

**DESEMBA**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 |
| 29 | 30 | 31 | | | | |

**Sikukuu za Tanzania - 2019**

| | |
|---|---|
| Jan 1 | Mwaka mpya |
| Jan 12 | Mapinduzi ya Zanzibar |
| Apr 7 | Kumbukumbu ya Karume |
| Apr 19 | Ijumaa Kuu |
| Apr 21 | Jumapili ya Pasaka |
| Apr 22 | Jumatatu ya Pasaka |
| April 26 | Siku ya Muungano |
| Mei 1 | Siku ya wafanyakazi |
| Jun 4 | Sikukuu ya Idi |
| Jul 7 | Saba Saba |
| Agosti 8 | Siku ya Wakulima |
| Agosti 11 | Sikukuu ya Idi |
| Okt 14 | Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere |
| Nov 9 | Sikukuu ya Maulid |
| Des 9 | Siku ya Uhuru |
| Des 25 | Sikukuu ya Krismasi |
| Des 26 | Siku ya kufungua zawadi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# 2020 Tanzania

**JANUARI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | |

**FEBRUARI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |

**MACHI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 |
| 29 | 30 | 31 | | | | |

**APRILI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | | |

**MEI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | | | | | | |

**JUNI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | 30 | | | | |

**JULAI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | |

**AGOSTI**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |
| 30 | 31 | | | | | |

**SEPTEMBA**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | | | |

**OKTOBA**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 |
| 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 |

**NOVEMBA**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 |
| 29 | 30 | | | | | |

**DESEMBA**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | | |

**Sikukuu za Tanzania - 2020**

| | |
|---|---|
| Jan 1 | Mwaka mpya |
| Jan 12 | Mapinduzi ya Zanzibar |
| Apr 7 | Kumbukumbu ya Karume |
| Apr 10 | Ijumaa Kuu |
| Apr 12 | Jumapili ya Pasaka |
| Apr 13 | Jumatatu ya Pasaka |
| April 26 | Siku ya Muungano |
| Mei 1 | Siku ya wafanyakazi |
| Mei 24 | Sikukuu ya Idi |
| Jul 7 | Saba Saba |
| Jul 31 | Sikukuu ya Idi |
| Agosti 8 | Siku ya Wakulima |
| Okt 14 | Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere |
| Okt 29 | Sikukuu ya Maulid |
| Des 9 | Siku ya Uhuru |
| Des 25 | Sikukuu ya Krismasi |
| Des 26 | Siku ya kufungua zawadi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

1. Andika majina ya miezi yenye siku 30.
2. Andika majina yenye siku 31.
3. Kuna Jumapili ngapi katika mwezi Julai mwaka huu.
4. Taja mwezi ambao mara nyingi shule hufungwa kwa ajili ya likizo ya mwisho wa mwaka.
5. Mwezi Februari mwaka huu una siku ngapi?

## Kazi ya kufanya: Siku yangu

Kujifunza zaidi kwa njia ya masomo ya mtandaoni kuandaa siku yangu

### Maelezo

Tumia programu ya kompyuta kuchora (kama vile Paint) ili kuandaa ratiba yako ya siku. Chora nyuso za saa za mshale na za kidigiti kuonesha shughuli zako za siku (kama vile muda wa kuamka, muda wa kwenda shule, muda wa kula na muda wa kulala).

## Jikumbushe

1. Katika uso wa saa, mshale mfupi huonesha saa, mshale mrefu huonesha dakika
2. Saa moja ni sawa na dakika 60
3. Muda hupimwa kwa siku, wiki, mwezi au mwaka

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Nusu saa | dakika 30 |
| Robo saa | dakika 15 |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la marudio

1. Chora nyuso za saa ya mshale kuonesha muda ufuatao:
   (a) Saa sita na robo (6:15)
   (b) Saa kumi kamili (10:00)
   (c) Saa mbili na nusu (2:30)
   (d) Saa tatu na dakika arobaini na tano (3:45)

2. Andika muda ufuatao kwa maneno:
   (a) 12:15 _____
   (b) 1:00 _____
   (c) 11:30 _____
   (d) 2:00 _____
   (e) 8:15 _____
   (f) 10:15 _____
   (g) 1:20 _____
   (h) 2:45 _____

3. Chagua maneno kutoka orodha B na yaandike katika orodha A ili yalete maana sahihi:

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (a) Dakika 90 | Unaonesha saa |
| (b) Mshale mrefu wa saa | Robo saa |
| (c) Mshale mfupi wa saa | Huonesha saa 12 |
| (d) Dakika 15 | Unaonesha dakika |
| (e) Dakika 30 | Dakika 60 |
| | Nusu saa |
| | Kasoro robo |
| | Saa moja na nusu |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Andika saa zifuatazo katika mtindo wa saa 12:

   (a) Saa 1930 (b) Saa 2324

   (c) Saa 2127 (d) Saa 1513

   (e) Saa 0712 (f) Saa 0835

5. Andika saa zifuatazo katika mtindo wa saa 24:

   (a) Saa 2:34 usiku (b) Saa 2:10 asubuhi

   (c) Saa 7:05 mchana (d) Saa 5:30 asubuhi

   (e) Saa 11:55 alfajiri (f) Saa 9:51 alasiri

   (g) Saa 9:15 alasiri (h) Saa 10:00 jioni

6. Saa 10:45 usiku ni saa ngapi katika mfumo wa saa 24?

7. Saa 1945 ni saa ngapi katika mtindo wa saa 12?

8. Kuna saa ngapi kuanzia 1500 mpaka saa 2300?

9. Kuna siku ngapi katika saa 72?

10. Je, mwaka huu ni mwaka mrefu au mfupi?

11. Andika jumla ya siku katika mwezi Juni, Julai na Agosti.

12. Katika mzunguko wa mwaka, andika miezi ambayo inafuatana na kila mmoja una siku 31.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sura ya Saba

# Fedha ya Tanzania

**Utangulizi**

*Katika sura hii utajifunza fedha ya Tanzania katika shilingi na senti. Vilevile, utajumlisha na kutoa fedha katika shilingi na senti. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia fedha ya Tanzania katika kufanya manunuzi, bajeti, kusimamia pesa na kuweka akiba.*

## Fedha ya Tanzania

*Fedha ya Tanzania ipo katika shilingi na senti. Thamani ya senti moja ni ndogo kuliko thamani ya shilingi moja. Shilingi moja ni sawa na senti mia moja. Senti huonekana zaidi katika maandishi kuliko upatikanaji wake katika matumizi ya kila siku. Fedha ya Tanzania pia ipo katika mfumo wa sarafu na noti zenye thamani mbalimbali.*

## Sarafu za Tanzania

*Sarafu za Tanzania ina thamani tofauti. Katika mzunguko wa fedha kuna sarafu za shilingi hamsini, mia moja, mia mbili na mia tano. Sarafu hizi zina alama za picha za marais, wanyama pori, vitu vya kihistoria na alama za kitaifa.*

**Mfano wa 1**

Sarafu ya shilingi 50 ya Tanzania ina rangi gani?

**Jibu**

Sarafu ya shilingi 50 ya Tanzania ina rangi ya dhahabu.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 2

*Je, utatofautisha vipi sarafu ya shilingi mia moja ya Tanzania na sarafu nyingine?*

**Jibu**

*Kila sarafu inaweza kutofautishwa kulingana na namba na alama zilizomo. Kwa mfano, sarafu ya shilingi mia moja imeandikwa "100" na swala wanne kwenye upande wake mmoja.*

## Mfano wa 3

Ni sarafu ipi ina picha ya Rais wa kwanza wa Tanzania?

**Jibu**

Sarafu ya shilingi mia moja.

## Zoezi la 1

Chunguza sarafu za Tanzania, kisha jibu maswali yanayofuata.

(a)







Shilingi _____

(b)







Shilingi _____

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c)







Shilingi _____

(d)







Shilingi _____

1. Je, kila sarafu ina thamani gani? Andika jibu katika nafasi iliyowazi katika kipengele (a) hadi (d).
2. Je, ni sarafu gani ina thamani kubwa kuliko zote?
3. Je, ni sarafu gani ina thamani ndogo kuliko zote?
4. Je, ni sarafu zipi umewahi kuziona?
5. Sarafu zipi umewahi kuzitumia?

## Noti za Tanzania

*Tanzania ina noti zenye thamani tofauti. Thamani ya kila noti imeandikwa kwa namba. Unaweza kuitofautisha noti moja na nyingine kwa kutumia alama mbalimbali zilizopo katika noti hizo.*

**Mfano**

Je, noti ya shilingi elfu kumi ina rangi gani?

**Jibu**

Noti ya shilingi elfu kumi ina rangi nyekundu

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

Chunguza noti hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.












FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE














FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Noti ipi ina thamani kubwa kuliko zote?
2. Noti ipi ina thamani ndogo kuliko zote?
3. Alama tatu zilizopo upande wa mbele wa noti ya shilingi elfu tano ni zipi?
4. Alama tatu zilizopo upande wa nyuma wa noti ya shilingi elfu mbili ni zipi?
5. Alama tano zilizopo katika noti ya shilingi elfu moja ni zipi?

## Zoezi la 3

Chunguza bei za bidhaa zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.

| Gharama | Bidhaa |
|---|---|
| 1,000/= |  Sahani |
| 4,000/= |  Samaki |
| 500/= |  Mboga za majani |
| 1,000/= |  Mkate |
| 5,000/= |  Sufuria |

1. Ni bidhaa ipi yenye bei kubwa kuliko zote?
2. Kati ya sahani na sufuria kipi chenye bei kubwa?
3. Ni bidhaa ipi yenye bei ndogo kuliko zote?
4. Ni bidhaa zipi zina bei sawa?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuandika fedha ya Tanzania katika shilingi na senti

Jinsi ya kuandika fedha kwenye shilingi, anza na neno shilingi, likifuatiwa na thamani. Vilevile, kwenye senti, anza na neno senti, kisha thamani. Katika numerali, thamani ya fedha ya shilingi na senti hutenganishwa na alama ya nukta.

### Mfano wa 1

(a) Je, shilingi 1 ni sawa na senti 50 ngapi?

**Njia**

(a) Sh 1 ni sawa na senti 100 au sh1 = st 100
st 50 ukiongeza nyingine st 50 unapata st 100
Kwa hiyo, shilingi 1 ni sawa na senti 50 mbili.

(b) Andika shilingi 500 na senti 50 kwa kifupi.

**Jibu**

(b) Kwa kifupi ni sh 500 st 50 au sh 500.50.

### Mfano wa 2

(a) Andika sh 700.00 kwa maneno.

(b) Andika sh 1200 na senti 70 kwa kifupi.

**Jibu**

(a) Shilingi 700.00 kwa maneno huandikwa shilingi mia saba.

(b) Sh 1200 na senti 70 kwa kifupi huandikwa sh 1200 na senti 70.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Senti 50 nne ni sawa na shilingi ngapi?
2. Soma, kisha andika kwa maneno fedha iliyoandikwa kwa kifupi katika jedwali lifuatalo. Kipengele (a) ni mfano.

| | **Fedha kwa kifupi** | **Fedha kwa maneno** |
|---|---|---|
| (a) | sh 5800 st 35 | Shilingi elfu tano mia nane na senti thelathini na tano |
| (b) | sh 75400 st 10 | |
| (c) | sh 23000 st 70 | |
| (d) | sh 632 st 37 | |
| (e) | sh 48350 st 05 | |
| (f) | sh 3600 st 00 | |
| (g) | sh 80495 st 95 | |
| (h) | sh 1750 st 50 | |
| (i) | sh 10000 st 00 | |
| (j) | sh 1100 st 20 | |

3. Soma kisha andika fedha kwa kifupi katika jedwali lifuatalo. Kipengele (a) ni mfano.

| | **Fedha kwa maneno** | **Fedha kwa kifupi** |
|---|---|---|
| (a) | Shilingi mia mbili na senti ishirini na tano | sh 200 st 25 |
| (b) | Shilingi mia tatu | |
| (c) | Shilingi elfu mbili mia mbili hamsini na senti hamsini | |
| (d) | Shilingi arobaini na tano elfu na senti thelathini | |
| (e) | Shilingi sabini na senti kumi | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Soma kisha andika fedha kwa kifupi katika jedwali lifuatalo. Kipengele (a) ni mfano.

| | Fedha kwa maneno | Fedha kwa kifupi |
|---|---|---|
| (a) | Shilingi hamsini na tano elfu na senti themanini na tano | Sh 55000 st 85 |
| (b) | Shilingi mia sita arobaini na senti tano | |
| (c) | Shilingi moja na senti hamsini | |
| (d) | Shilingi tisini na tisa elfu mia nane na senti tisini | |
| (e) | Shilingi hamsini na senti sitini | |

5. Mshahara wa Rozi ni shilingi 315,000 na senti 80 kwa siku. Andika mshahara huo kwa kifupi.

## Kujumlisha fedha

Unapojumlisha fedha zinazohusisha shilingi na senti zingatia kuwa shilingi moja ni sawa na senti 100.

**Mfano wa 1**

sh 500 st 20 + sh 380 st 70 =

**Hatua**

1. Jumlisha senti: st 20 + st 70 = st 90. Andika st 90 katika nafasi ya senti.
2. Jumlisha shilingi: sh 500 + sh 380 = sh 880. Andika sh 880 katika nafasi ya senti.

   Kwa hiyo, jibu ni sh 880 st 90

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 2

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 4596 | 65 |
| + | 3987 | 75 |
| | | |

**Hatua**

1. Jumlisha senti: 65 + 75 = st 140
   Badili st 140 kuwa sh1 na st 40. Kisha andika st 40 katika nafasi ya senti na jumlisha sh 1 katika shilingi

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 4596 | 65 |
| + | 3987 | 75 |
| | | 40 |

2. Jumlisha shilingi:
   1 + 4596 + 3987 = 8584.
   Andika sh 8584 katika nafasi ya shilingi

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 4596 | 65 |
| + | 3987 | 75 |
| | 8584 | 40 |

Kwa hiyo, jibu ni sh 8,584 st 40.

## Mfano wa 3

| | | |
|---|---|---|
| | sh | 11650 |
| + | sh | 78450 |
| | | |

**Njia**

| | | |
|---|---|---|
| | sh | 11650 |
| + | sh | 78450 |
| | sh | 90100 |

Kwa hiyo, jibu ni sh 90,100.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. sh 5000 + sh 4000 =
2. sh 2438 + sh 4326 =
3. sh 1326 + sh 1318 =
4. sh 625445 st 50 + sh 357223 st 85 =
5. sh 14955 st 50 + sh 4955 st 55 =
6. sh 423293 st 45 + sh 549314 st 45 =
7. 
| | |
|---|---|
| | sh 4521 |
| + | sh 2183 |
| | |

8. 
| | |
|---|---|
| | sh 1326 |
| + | sh 2788 |
| | |

9. 
| | sh | st |
|---|---|---|
| | 625 | 45 |
| + | 364 | 20 |
| | | |

10. 
| | sh | st |
|---|---|---|
| | 5001 | 80 |
| + | 4999 | 45 |
| | | |

11. 
| | sh | st |
|---|---|---|
| | 1060 | 05 |
| + | 2175 | 15 |
| | | |

12. 
| | sh | st |
|---|---|---|
| | 714370 | 80 |
| + | 3056 | 35 |
| | | |

13. 
| | sh | st |
|---|---|---|
| | 433270 | 55 |
| + | 433865 | 45 |
| | | |

14. 
| | sh | st |
|---|---|---|
| | 385534 | 05 |
| + | 453057 | 45 |
| | | |

15. 
| | |
|---|---|
| | sh 60250 |
| + | sh 28970 |
| | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mafumbo yenye dhana ya kujumlisha fedha

### Mfano wa 1

Sabina aliuza kuku wawili. Kuku wa kwanza aliuzwa kwa sh 33,620 na wa pili aliuzwa kwa shilingi 22,350. Je, Sabina alipata fedha kiasi gani?

**Njia**

| | | |
|---|---|---|
| | sh | 33620 |
| + | sh | 22350 |
| | sh | 55970 |

Kwa hiyo, Sabina alipata kiasi cha sh 55,970.

### Mfano wa 2

Mapunda alitumia shilingi 245,950 kwa mwezi kununua maziwa na shilingi 152,850 kwa kulipia usafiri. Jumla alitumia kiasi gani cha fedha?

**Njia**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Maziwa | | sh | 245950 |
| Usafiri | + | sh | 152850 |
| | | sh | 398800 |

Kwa hiyo, Mapunda alitumia jumla ya shilingi 398,800.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

1. Saidi aliamua kuuza kuku wawili. Kuku wa kwanza aliuzwa kwa sh 13,600 na wa pili aliuzwa kwa Sh 16,250. Je, Saidi alipata fedha kiasi gani?
2. Muuza mboga alipata noti za shilingi 5000, 2000, 1000 na sarafu ya shilingi 200 baada ya mauzo ya mboga. Tafuta jumla ya fedha alizopata.
3. Yohana aliuza mayai kwa shilingi 8,600 na kuku kwa shilingi 17,500. Je, alipata jumla ya shilingi ngapi?
4. Maria aliweka akiba ya fedha benki kiasi cha shilingi 230,000. Ikiwa benki ilimwongezea shilingi 4,550 na senti 75 kama faida. Je, Maria atakuwa na jumla ya akiba ya shilingi ngapi?
5. Kikundi fulani cha vijana kilianzisha mradi wa kufuga nyuki. Kilitumia shilingi 42,400 kuandaa mizinga na shilingi 48,200 kununulia vifaa vya kurina asali. Je, kilitumia kiasi gani cha fedha kuanzisha mradi huo?
6. Mpishi alinunua gunia la mkaa kwa shilingi 43,350 na gunia la mahindi kwa shilingi 55,600. Jumla alilipa kiasi gani cha fedha?
7. Mwanafunzi alinunua kitabu cha Hisabati kwa shilingi 9,500 na daftari za shilingi 2,600. Je, alitumia kiasi gani cha fedha katika manunuzi yake?
8. Bupe alinunua mchele kwa shilingi 438,000. Baada ya kuuza alipata faida ya shilingi 96,000. Je, aliuza mchele kwa shilingi ngapi?
9. Jeni alipata hasara ya shilingi 2,500 baada ya kuuza bidhaa kwa shilingi 87,500. Je, bidhaa hiyo ilikuwa imenunuliwa kwa kiasi gani?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

10. Juhudi alipata zawadi ya shilingi 52,500 baada ya kufaulu mtihani wa Hisabati. Pia, mama yake alimpatia shilingi 21,700. Iwapo Juhudi alikuwa na shilingi 18,550 kabla ya zawadi, je, jumla alikuwa na kiasi gani cha fedha?

## Kutoa fedha

Tendo la kutoa fedha hufanyika kama kutoa namba nzima kwa kuanzia kulia kwenda kushoto.

### Mfano wa 1

sh 48 965 st 95 – sh 25 843 st 85 =

**Hatua**

1. Toa senti: 95 – 85 = st 10. Andika senti katika nafasi ya senti
2. Toa shilingi: 48 965 – 25 843 = sh 23122. Andika shilingi katika nafasi ya shilingi.

   Kwa hiyo, jibu ni sh 23 122 st 10.

### Mfano wa 2

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 83721 | 85 |
| – | 61510 | 40 |
| | | |

**Hatua**

Toa senti: 85 – 40 = st 45

Andika st 50 katika nafasi ya senti

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 83721 | 85 |
| – | 61510 | 40 |
| | | 45 |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Toa shilingi:
83721 – 61510 = sh 22211
Andika sh 22211 katika nafasi ya shilingi

Kwa hiyo, jibu ni sh 22211 st 45.

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 83721 | 85 |
| – | 61510 | 40 |
| | 22211 | 45 |

## Mfano wa 3

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 869335 | 30 |
| – | 427123 | 70 |
| | | |

**Hatua**

1. Toa senti: 30 – 70 haitoshelezi.
   Chukua shilingi moja kutoka katika shilingi 5 badili kuwa na st 100.
   Jumlisha senti: 100 + 30 = st 130.
   Toa senti: 130 – 70 = st 60
   Andika st 60 katika nafasi ya senti

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 869335 | 30 |
| – | 427123 | 70 |
| | | 60 |

   Kumbuka umechukua shilingi 1 kwenye shilingi 5.
   Hivyo, umebakiwa na shilingi 4.

2. Toa shilingi:
   869334 – 427123 = sh 442211
   Andika sh 442211 katika nafasi ya shilingi

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 869335 | 30 |
| – | 427123 | 70 |
| | 442211 | 60 |

   Kwa hiyo, jibu ni sh 442,211 st 60.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mfano wa 4

sh 4180
– sh 2494

**Njia**

sh 4180
– sh 2494
sh 1686

Kwa hiyo, jibu ni sh 1,686.

## Zoezi la 7

1. sh 4561 – sh 2364 =
2. sh 5751 – sh 4030 =
3. sh 7 620 – sh 5245 =
4. sh 90900 – 75300 =
5. sh 58675 – sh 39248 =
6. Sh 89990 – sh 68990 =
7. sh 914955 st 60 – sh 612950 st 05 =
8. sh 870300 st 40 – sh 413200 st 25 =

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

9. sh 4330
− sh 1215

10. sh 6779
− sh 4125

11. sh 80560
− sh 60590

12. sh 99100
− sh 65700

13. sh 75750
− sh 25920

14. sh 35000
− sh 20090

15. sh 21800
− sh 15350

16. sh 42300
− sh 18800

17.

| sh | st |
|---|---|
| 720561 | 65 |
| − 310340 | 40 |

18.

| sh | st |
|---|---|
| 564868 | 25 |
| − 19853 | 75 |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

19.

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 867662 | 20 |
| − | 453221 | 10 |

20.

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 954330 | 30 |
| − | 623220 | 10 |

21.

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 21201 | 10 |
| − | 11102 | 60 |

22.

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 68654 | 14 |
| − | 18129 | 14 |

23.

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 4500 | 80 |
| − | 180 | 45 |

24.

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 100 | 10 |
| − | 90 | 20 |

25.

| | sh | st |
|---|---|---|
| | 945601 | 70 |
| − | 431102 | 60 |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mafumbo yenye dhana ya kutoa fedha ya Tanzania

### Mfano wa 1

Anna alikuwa na shilingi 80,800. Alitumia shilingi 20,000 kununua sare za shule na shilingi 17,500 kununua madaftari. Je, Anna alibakiwa na kiasi gani cha fedha?

**Njia**

| | | |
|---|---|---|
| Sare za shule: | | sh 20000 |
| Madaftari: | + | sh 17500 |
| | | sh 37500 |

Anna alitumia jumla ya shilingi 37,500 kununulia sare za shule na madaftari.

Chukua kiasi alichokuwa nacho, toa kiasi alichotumia.

| | | |
|---|---|---|
| Kiasi alichokuwa nacho: | | sh 80800 |
| Jumla aliyotumia: | – | sh 37500 |
| | | sh 43300 |

Kwa hiyo, Anna alibakiwa na shilingi 43,300.

### Mfano wa 2

Petro aliuza ng'ombe mmoja kwa shilingi 450,000 siku ya mnada. Baada ya mnada alimpa mtoto wake kiasi cha shilingi 215,000 kwa ajili ya mahitaji ya shule. Je, Petro alibakiwa na kiasi gani?

**Njia**

| | | |
|---|---|---|
| Bei ya ng'ombe: | | sh 450000 |
| Kiasi alichotoa: | – | sh 215000 |
| | | sh 235000 |

Petro alibakiwa na sh 235,000.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8

1. Halima alikwenda dukani na shilingi 5,000 kununua sukari. Alinunua sukari kilo moja kwa shilingi 3,325. Je, Halima alirudi nyumbani na shilingi ngapi?
2. Musa alipata faida ya shilingi 2,070 baada ya kuuza mahindi kwa shilingi 97,650. Je, alinunua mahindi hayo kwa shilingi ngapi?
3. Bahati alikuwa na shilingi 10,000. Aliwapatia watoto wake wawili fedha hiyo kwa ajili ya nauli. Iwapo alimpatia mtoto mmoja shilingi 4,600, mtoto wa pili alimpatia shilingi ngapi?
4. Rehema alikuwa na shilingi 75,000 na alitumia shilingi 31,650. Je, Rehema alibakiwa na shilingi ngapi?
5. Seif alichukua shilingi 85,000 katika akiba yake iliyo kuwa benki. Alilipia umeme wa shilingi 50,449 na senti 25 na maji shilingi 15,000 na senti 75. Je, Seif alibakiza kiasi gani cha fedha?
6. Mwanaheri alipewa sh 60,000 na baba yake kwa ajili ya kununua mahitaji ya shule. Iwapo alinunua madaftari kwa sh 31,500 na kitabu kwa sh 8,500. Je, Mwanaheri alibakiwa na shilingi ngapi?
7. Safina alipewa shilingi 1,000 kwa matumizi ya shule. Akanunua maji ya shilingi 450 na chapati ya shilingi 300. Je, Safina alibakiwa na shilingi ngapi?
8. Pendo alikuwa na shilingi 90,000. Alinunua mashuka mawili kwa shilingi 32,500 na gauni kwa shilingi 40,000. Je, alibakiwa na shilingi ngapi?
9. Josefu alikuwa na shilingi 350,000. Alitumia shilingi 127,500. Je, alibakiwa na shilingi ngapi?
10. Fabian alinunua runinga kwa shilingi 435,250. Baadae akaiuza kwa shilingi 582,950. Je, alipata kiasi gani cha fedha zaidi ya bei aliyonunulia?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya

Kujifunza zaidi juu ya fedha ya Tanzania kwa njia ya masomo mtandaoni

## Maelezo

Tumia masomo ya mtandaoni kujifunza hesabu za kujumlisha na kutoa fedha katika shilingi na senti.

## Jikumbushe

1. Unapotenga shilingi na senti katika tarakimu, senti huandikwa kwa tarakimu mbili
2. Senti mia moja ni sawa na shilingi moja
3. Unapojumlisha na kutoa fedha, anza na senti kisha shilingi
4. Fedha ya Tanzania ipo katika sarafu na noti zenye thamani mbalimbali
5. Fedha hutumika wakati wa kufanya malipo. Aidha, huonesha thamani ya vitu kwa njia ya bei

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Noti | Fedha iliyotengenezwa kwa kipande cha karatasi maalumu. |
| Sarafu | Fedha iliyotengenezwa kwa kutumia madini. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la Marudio

Chunguza noti zifuatazo, kisha jibu swali la 1 hadi 3.

(a)







(b)



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




1. Taja majina ya noti (a) na (b).
2. Taja alama tatu zilizopo katika noti (a)
3. Taja alama tatu zilizopo katika noti (b)
4. Andika kiasi cha fedha zifuatazo kwa kifupi:

| Fedha kwa maneno | Fedha kwa kifupi |
|---|---|
| (a) Shilingi elfu moja mia moja na senti ishirini | |
| (b) Shilingi mia sita arobaini na senti tano | |

5. sh 600 + sh 400 =
6. sh 4000 + sh 3700 =
7. sh 8700 + sh 900 =
8. sh 450 + sh 7300 + sh 100 =
9. sh 25300 + sh 60200 =
10. sh 52670 + sh17380 =
11. sh 11500 + sh 80150 =

Mfano
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

12. sh 36800 + sh 44000 =

13. sh 63435 st 10 – sh 8375 st 65 =

14. sh 145489 st15 – sh 51432 st 45 =

15. sh 32456 st 10 + sh 63367 st 65 =

16. sh 25445 st 50 + sh 57223 st 85 =

17. sh 7535 – sh 6025 =

18. sh 4050 – sh 2500 =

19. sh 392450 – sh 138510 =

20. sh 174000 – sh 35600 =

21.
sh 6430
– sh 5240
_____

22.
sh 9883
– sh 3265
_____

23.
sh st
90527 85
– 30210 80
_____

24.
sh st
71171 00
– 15101 50
_____

25.
sh st
67501 70
– 35322 35
_____

26.
sh st
868660 45
– 534330 15
_____

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

27.
| | sh | |
|---|---|---|
| | 27800 | |
| + | 39400 | |
| | | |

28.
| | sh | st |
|---|---|---|
| | 156280 | 15 |
| + | 138270 | 30 |
| | | |

29.
| | sh | |
|---|---|---|
| | 70880 | |
| + | 16970 | |
| | | |

30.
| | sh | st |
|---|---|---|
| | 178850 | 45 |
| + | 235112 | 55 |
| | | |

31.
| | sh | st |
|---|---|---|
| | 5075 | 05 |
| + | 3350 | 50 |
| | | |

32.
| | sh | st |
|---|---|---|
| | 263009 | 65 |
| − | 124087 | 55 |
| | | |

33. *Suzana alipata shilingi 5,380 siku ya Jumamosi na shilingi 2,010 siku ya Jumatatu. Je, jumla alipata shilingi ngapi?*

34. *Paza hutumia shilingi 45,000 kwa mwezi kununua maziwa na shilingi 52,500 kwa usafiri. Jumla hutumia kiasi gani cha fedha?*

35. *Obedi anahitaji shilingi 5,500 ili aweze kununua viatu. Ikiwa ana shilingi 2,600, amepungukiwa shilingi ngapi ili aweze kununua viatu hivyo?*

36. *Diana alinunua mbuzi kwa shilingi 55,000 na akamuuza kwa shilingi 70,500. Je, alipata faida kiasi gani?*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

37. Safina alipewa shilingi 1,000 kwa matumizi ya shule. Alinunua maji kwa shilingi 500 na pipi za shilingi 250. Safina alibakiwa na shilingi ngapi?

38. Nasibu alitoa noti ya shilingi 10,000 kulipia nauli ya basi kiasi cha shilingi 6,500. Alirudishiwa kiasi gani cha fedha?


39. Mwezi uliopita Skola aliweka akiba ya shilingi 5,600 na mwezi huu tayari ameweka shilingi 2,500. Je, mpaka sasa ana kiasi gani cha fedha?


40. Ali alitumia shilingi 25,000 kununua viatu, shilingi 30,000 kwa ajili ya nauli na shilingi 45,000 kwa ajili ya sare. Je, jumla alitumia shilingi ngapi?


FOR ONLINE USE ONLY

# Vitabu vingine kutoka
# Taasisi ya Elimu Tanzania

## Darasa la Tatu





















ISBN 978-9987-09-996-2